SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

ACT WAZALENDO

UKURASA 3

## ACT yaanika majina wasemaji wa kisekta




UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Februari 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580849
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Wataka waziri apokwe nguvu Sheria ya Ugaidi

**PIA** wapendekeza polisi wanaofanya operesheni za kificho kushtakiwa...*Endelea ukurasa 2 & 7*



Rais Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kwa Daktari wa Kitengo cha Magonjwa ya Figo katika Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere mkoani Mara, Dk. Ridhiwani Said, kuhusu maendeleo ya utoaji wa huduma, alipotembelea kukagua ujenzi wa hospitali hiyo, Kijiji cha Kwangwa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Mjini mkoani Mara jana. **PICHA: IKULU**

## WanaCCM 11 wajitokeza kuomba uteuzi unaibu spika


UKURASA 3

## Samia aagiza vigogo h/shauri kusimamishwa tuhuma ufisadi

UKURASA 2

**MICHEZO** NABI ABEBA LAWAMA MECHI NA MBEYA CITY UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Meneja Mradi wa Shirika la Green Community Initiatives (GCI), George Nyanda, akitoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kata ya Nyida na Puni katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kabla ya kuunda madarasa ya watoto yatakayoshirikisha washiriki 240 kutoka vijiji sita na kata mbili wakati wa utekelezaji wa mradi wa ukatili wa kijinsia kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT) jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wataka waziri apokwe nguvu Sheria ya Ugaidi

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimependekeza kuondolewa kifungu kinachompa mamlaka Waziri wa Mambo ya Ndani kutunga kanuni na kumtangaza mtu kuwa gaidi wa ndani.

Mapendekezo hayo yalitolewa na Ofisa Uchechemuzi wa LHRC, Willium Maduhu, katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Maduhu, alisema kabla ya kupitisha vifungu hivyo ni vyema wabunge wakaviangalia kwa jicho la ziada, vinginevyo watasababisha madhara makubwa kwa nchi.

Aidha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi akiruhusiwa kumtangaza mtu kama gaidi wa ndani ya nchi kuna madhara makubwa yanayoweza kutokea.

"Sheria mama imetoa mamlaka kumtangaza mtu au kikundi kama gaidi wa kimataifa, sasa kwa mapendekezo haya waziri anapewa mamlaka ya kumtangaza mtu yeyote kuwa gaidi wa ndani, kwamba kanuni za Umoja wa Mataifa (UN) zitatumika,"alisema na kuongeza:

"Pia kifungu kinasema waziri atatunga kanuni za namna ya kumtangaza mtu kama gaidi, sasa kama unasema utatumia kanuni za Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwanini unampa waziri mamlaka ya kutunga kanuni. Nchi inapambana kukuza uchumi sasa ukipata mwekezaji/mtalii hawezi kuja kwenye nchi ambayo kuna mtu/watu wametangazwa kuwa magaidi," alisema.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kutangaza nchi kuwa ina magaidi taasisi za fedha kimataifa hazitaleta fedha jambo ambalo litaathiri uchumi.

Maduhu alisema kanuni zinatungwa na waziri ambaye ataweka vigezo vya mtu kutangazwa gaidi na kwamba wakati anatekeleza hayo wawakilishi wa wananchi (wabunge) hawatashirikishwa.

Alisema nchi za Kenya, Burundi na Rwanda wana sheria ya ugaidi ambayo ina kifungu cha kumtangaza mtu kuwa gaidi wa kimataifa na si kumtangaza kuwa wa kitaifa.

Aidha, alisema kifungu hicho pia hakijafafanua kuwa watakaotangazwa na waziri ni raia pekee au hata wageni.

Maduhu alisema ni muhimu kujiuliza anayetangazwa gaidi wa ndani anakuwa yuko gerezani au kituo cha polisi, kwa kuwa sheria za kimataifa ni ngumu sana.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Hamad Masauni

"Haya umemtangaza mtu ni gaidi kwenye gazeti la serikali halafu mahakama inasema siyo gaidi unafanyaje? Unamfidia au? Tuliangalie kimataifa, kimataifa unatengwa na dunia nzima, hapa haki za wengi zitavunjwa."

Maduhu alisema sheria hiyo inazungumzia mambo kama kumtisha mtu ambako kunasababisha hofu kwa umma, ukimvamia mtu na ukasababisha kifo, ukitumia vilipuzi imetafsiriwa ni ugaidi.

"Tunapendekeza kifungo chote cha pili kiondolewe, tukiacha hivi tutawapa shida waendesha mashtaka kuthibitisha kwamba kauli husika ilikuwa ni vitisho na ilisababisha hofu kwa umma, itabidi umuite mtu mmoja mmoja umuulize jana uliogopa? Ulipata hofu? Jambo ambalo ni gumu," alisema.

Aidha, alisema mapendekezo hayo yanaeleza ukiwasumbua polisi, idara ya maji, Shirika la Umeme (TANESCO), madaktari inahesabika ni ugaidi. "Kwa mujibu wa mapendekezo haya maandamano na migomo hayatafsiriwa kama ugaidi isipokuwa kama hayajasababisha kifo, cha kujiuliza yakisababisha kifo bila kujali nani kasababisha itahesabiwa na ugaidi...tunapendekeza kifungu hiki kiondolewe kwa kuwa kinakinzana na ibara ya 20 ya katiba inayotoa uhuru wa kukusanyika," alibainisha Maduhu.

Alisema kesi nyingi za ugaidi walizofunguliwa watu wengi waliachiwa na mahakama, jambo, ambalo ni lazima kufikiri sana kabla ya kupitisha sheria hiyo.

# Samia aagiza vigogo h/shauri kusimamishwa tuhuma ufisadi

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza kusimamishwa kazi wakuu wa idara ya fedha, mipango na manunuzi katika Halmashauri ya Bunda Vijijini mkoani Mara kupisha uchunguzi kutokana ujenzi wa jengo la makao makuu ya halmshauri ya wilaya hiyo kusuasua licha ya Sh. milioni 400 kutumika.

Rais aliyasema hayo jana mjini Musoma baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

"Lakini fedha Sh. milioni 400 zimeshatumika, ukienda pale kwenye halmashauri hakuna kilichoko, kuna nondo zimesimama na mashimo yamechimbwa, nimeuliza kwa nini wanasema vifaa havijasogezwa kwa kuwa hakuna ghala ya kuhifadhia vifaa," alisema na kuongeza:

"Lakini naambiwa ujenzi unasua sua, lakini wakuu wote wa idara wapo hapo, DC yupo hapo, DED yupo hapo, wakuu wa idara wako wapo, lakini hili la milioni 400 kutumika na vitu havipo mheshimiwa Mkuu wa Mkoa naomba wahusika waliohusika na haya, nadhani atakuwa ni mkuu wa kitengo au idara ya fedha, mipango na watu wa manunuzi, wakae pembeni wapishe uchunguzi."

Rais pia alimwamuru Mkuu wa Mkoa huo, Ally Happi, kusitisha mkataba na mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya makutano ya juu mpaka Sanzate wa kilomita 50, ulioanza mwaka 2013 na kugharimu Sh. bilioni 54.5 hadi leo haujakamilika.

"Mkandarasi hana vifaa vya kufanyia kazi, lakini hana fedha za kufanyia kazi, anasubiri serikali ilipe ndiyo afanye kazi, sasa makandarasi wa aina hii Mkuu wa Mkoa (Happi) iwe mwisho... Mheshimiwa Mkuu wa mkoa vunja huo mkataba na muanze upya," alisema Rais.

Sakata hilo lilianzia kwa Ally Happi alipopata nafasi ya kumshukuru Rais kwa kuwapelekea fedha ya kuendeleza miradi ya maendeleo katika mkoa huo ambapo alimwomba kubadilisha wakuu wa idara katika Halmashauri za Bunda Vijijini, Tarime Vijijini na Musoma Vijijini kutokana na kutowajibika ipasavyo.

"Mheshimiwa Rais, ninakuomba, ipo haja ya kufumua wakuu wa idara, tumebadilisha wakurugenzi, umetusaidia, umetubadilishia wakuu wa wilaya, lakini wale watendaji wanaowasaidia wakurugenzi sehemu zote nilizozitaja wananuka rushwa," alisema Happi.

**UMMY ASHTUKIA UFISADI**

Katika hatua nyingine Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alimwomba Rais Samia kutowapa Sh. bilioni 23 zilizoombwa kuendeleza ujenzi wa hospitali hiyo mpaka wajiridishe fedha hizo zinatatumikaje.

"Mheshimiwa Rais, usitupe hizo fedha kwanza mpaka nitakapojiridhisha fedha hizi bilioni 24 zinakwenda kufanya nini, kwa sababu walituchomekea zilisemwa zinahitajika Sh. bilioni 27, nikamwelekeza katibu mkuu wangu na yeye amefuatilia tukakuta fedha zinazohitajika ni labda Sh. bilioni 24 na nimeshamwelekeza katibu mkuu awapeleke TAKUKURU wote waliohusika kuongeza makisio ya ujenzi wa hospitali hii," alisema Ummy.

**DAWA HAKUNA**

Waziri huyo alisema kuwa licha ya Rais kutoa Sh. bilioni 333. 8 kwa ajili ya kununulia dawa, vifaa na vifaa tiba, lakini upatikanaji wa dawa katika vituo vya serikali nchini hauridhishi.

"Mheshimiwa Rais napenda niseme ukweli mbele yako, licha ya kwamba umetupatia fedha ya dawa, hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vyetu vya dawa hainiridhishi, haifurahishi, wananchi wakienda wanaambia hakuna panadol wala antibiotic.

Kwenye makaratasi wataalamu wangu wameniambia dawa zipo asilimia 90 mheshimiwa Rais nimekataa, nimemwambia katibu mkuu afanye 'tracer medicine' dawa 30, mheshimiwa Rais naona tunajipima kidogo, tupime dawa zote muhimu ambazo mwananchi anatakiwa kuzipata," alisema Ummy.

"Nimeona watendaji wangu wameniambia kuwa upatikanaji wa dawa ni wa asilimia 98, nimekataa hii si kweli."

## HABARI KITAIFA

# WanaCCM 11 wajitokeza kuomba uteuzi unaibu spika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WABUNGE 11 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamechukua na kurudisha fomu za kuomba ridhaa ya kuteuliwa na chama kugombea unaibu spika wa Bunge.

Hadi kufikia jana saa 10 jioni waliochukua na kurudisha fomu ni Mbunge wa Ilala Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Nzega Vijijini, Hamis Kigwangalah pamoja na Mbunge wa Mahonda Mkoa wa Kaskazini Ugunja, Abdullah Ali Mwinyi.

Wengine ni Mbunge wa Hanang', Samweli Xaday, Mbunge wa Mwanga Joseph Anania, Mbunge wa Mufindi Kusini, David Kihenzele pamoja na Mbunge wa Muleba Kusini, Dk. Oscar Kikoyo.

Mbali na hao wengine ni Mbunge wa Kilombero, Abubakar Asenga, Mbunge wa Maswa Mashariki, Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Korogwe Vijijini, Timotheo Mnzava pamoja na Mbunge wa Kigoma Mjini, Kirumbe Ng'enda.

Akizungumza wakati wa kufunga uchukuaji wa fomu pamoja na urudishaji, Katibu wa NEC Organaizesheni, Dk. Maudline Castico, alisema ratiba ya vikao vya kitaifa vya CCM ambavyo ni Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Zanzibar, Sekretarieti ya Halmashauri ya CCM Taifa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa vitaendelea kulingana na ratiba iliyotolewa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka.

"Nipende kuchukua fursa hii kuwapongeza wanachama wote waliojitokeza kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hii,"alisema Dk. Castico.

Aidha, alisema chama kinamshukuru Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan na Katibu Mkuu, Daniel Chongolo kwa namna wanavyoendelea kuimarisha na kusimamia demokrasia ndani ya chama.

Awali akizungumza baada ya kurudisha fomu Mbunge wa Mahonda, Abdullah Ali Mwinyi alisema hana mambo mengi ya kuzungumza na waandishi bali anaendelea kusubiri maamuzi ya vikao vinavyofuata vya chama.

Alisema: "Leo nimefanikiwa kurudisha fomu baada ya jana kuchukua kwenda kujaza. Lakini sina mengi naendelea kusubiri maamuzi ya vikao vinavyofuata vya chama," alisema.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na CCM, leo Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa itawajadili wagombea hao na kuishauri Kamati Kuu Taifa, majina ya wagombea.

Pia Februari nane, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, kuchuja na kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea, na Februari 10, mwaka huu, kamati ya wabunge wa CCM watapiga kura.

TANGAZO!!
AFRIWELD INDUSTRIES LTD
Nafasi ya kazi

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35
**Nafasi:** Mauzo
MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!!
wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!
Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**
Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni
**01/01/2022 MPAKA 15/02/2022**
**Asante**
116653602

# Wasemaji wa kisekta wa ACT watangazwa

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha ACT- Wazalendo kimetangaza wasemaji wa kisekta katika wizara mbalimbali zinazounda serikali, pamoja na mambo mengine watakuwa na wajibu wa kuishauri serikali na kupendekeza sera mbadala kwa weledi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema ACT-Wazalendo kupitia vikao vyake na katika utekelezaji wa mpango mkakati wa chama kuelekea mwaka 2025 kutekeleza dhana hii kwa muktadha wa sasa wa Tanzania nje ya Bunge.

Alisema wasemaji wa kisekta hao watakuwa na wajibu wa kutoa sera mbadala dhidi ya sera zinazotekelezwa sasa na chama tawala.

Zitto alisema: "Kila msemaji wa kisekta atakuwa msimamizi wa waziri katika serikali husika. Kamati hii ya kuisimamia serikali itasaidiwa kazi zake na sekretarieti ambayo itakuwa na kazi kubwa ya kufanya utafiti na kuzalisha serikali mbadala."

Aliongeza: "Kwa njia hii tutaweza kufanya kazi ya wananchi ya kuwa wasemaji wao, kuibua masuala muhimu ya wananchi na kuyatolea mapendekezo ya majawabu."

Zitto alisema dhana ya wasemaji wa kisekta ni dhana komavu katika nchi zinazofuata utamaduni wa Jumuiya ya Madola katika siasa za demokrasia ya vyama vingi, na imekuwa ikitumika zaidi katika mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola ikiwamo Tanzania.

Zitto aliongeza: "Kwa muda mrefu sana siasa za Tanzania zimekuwa ni siasa 'unapinga nini' badala ya siasa za 'unapendekeza nini', wasemaji wa kisekta watafanya ukosoaji na vile vile kupendekeza nini tutafanya kama tungekuwa tunaunda serikali."

Zitto alisema itakuwa ni wajibu wa wasemaji wa kisekta kuishauri serikali kisera na kiutendaji na vile vile kuisimamia kwa kukosoa sera ambazo zina madhara kwa Watanzania na Taifa.

Zitto aliwataja wasemaji hao kuwa ni Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Msemaji Mkuu wa Baraza Kivuli, Abdul Nondo, Fedha na Uchumi- Emanuel Mvula, Mambo ya Nje - Fatma Fereji, Ulinzi- Masoud Salim, Mambo ya Ndani - Mbarala Maharagande, Elimu - Riziki Shahari Mngwali, Afya - Dk. Elizabeth Sanga, Uwekezaji, Mashirika ya Umma na Hifadhi ya Jamii - Mwanaisha Zuberi Mndeme.

Zingine ni Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Muungano - Pavu Juma Abdallah, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Maendeleo vijijini - Kulthum Mchuchuli.

Wengine ni Msemaji wa Wizara ya Nishati - Isihaka Mchinjita, Madini - Edgar Mkosamali, Viwanda na Maendeleo ya Biashara - Halima Nabalang'anya, Maji na Mazingira - Esther Thomas, Katiba na Sheria -Victor Kweka, Kilimo, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi - Mtutura A. Mtutura.


Furahia Urafiki wa Faida
Akaunti inayorahisisha na kuboresha umoja wenu katika kufikia malengo yenu
Unachostahili ni URAHISI
Niamoja ACCOUNT
CRDB BANK Tunakusikiliza
166924



Miongoni mwa nyumba za makazi ya polisi Kunduchi mkoani Dar es Salaam, baada ya ujenzi wake kukamilika hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machinga soko la Karume walalamikia maeneo mapya

**Na Jenifer Gilla**

BAADHI ya machinga katika Soko la Mchikichini, Karume waliopewa maeneo mapya ya kufanyia biashara baada ya mwanzo kuachwa wazi ili kupisha barabara, wamelalamikia maeneo hayo kuwa yana kasoro ambazo hazifai kwa shughuli zao.

Kaiza Khenga (36), alisema kibanda kipya alichopewa ni kidogo na hakitoshi kuweka biashara zake tofauti na kibanda alichokuwa anatumia mwanzo kabla ya soko hilo kuungua.

"Hii meza niliyopewa ya futi nne ni ndogo sana kwa biashara yangu ya viatu kwa sababu vinakuwa vingi, hapa ninalazimika kuweka viatu kama pea 50 tu wakati balo zima lina pea karibu 400, meza yangu ya mwanzo ilikuwa na ukubwa wa futi sita sawa na mita mbili," alisema Kaiza.

Naye Faidini Ramadhani, alisema licha ya meza hizo kuwa ndogo, eneo hilo si salama kwa biashara zao kwa sababu ya miundombinu yake kutokuwa rafiki kwani mvua zinaponyesha kunajaa maji, hivyo kuathiri shughuli zao.

"Hapo mwanzo hili eneo lilikuwa halikai mfanyabiashara yeyote kwa sababu mvua zinaponyesha maji ya kutoka huko juu yote yanapita hapa, wateja hawawezi kuja huku kipindi cha mvua, tunaomba, hii ni hasara kwetu kwa sababu itatulazimu kufunga biashara kipindi chote cha mvua, tutahudumiaje familia zetu," alilalamika Faidina.

Dennis Mmari, muuza viatu , alisema kwa muda mfupi aliokaa kwenye vibanda hivyo mauzo yake yamekuwa madogo tofauti na eneo lake la mwanzo kutokana na eneo hilo kuwa sehemu iliyojificha hivyo wateja wake waliomzoea bado hawajafika.

"Kwa ufupi huku biashara ni ngumu, kutokana nimeletwa kwenye eneo ambalo limejificha na wateja wangu bado hawajakuzoea, kwa hivyo tunalazimika kwenda kwenye maeneo yetu ya mwanzo kushawishi wateja waje huku nyuma ni kazi sana," analalamika Dennis.

Nao wafanyabiashara ambao hawajapatiwa maeneo ya kukaa mpaka sasa, walilalamika kuchelewa kupata maeneo hayo kunawafanya kuishi maisha magumu kwa kuwa hawaingizi fedha za kuhudumia familia zao.

Khamisi Mpachuka mfanyabiashara wa pochi, alisema helewi mwelekeo wa biashara yake katika eneo hilo huku maisha yake yakiendelea kuzorota kutokana na kutofanya biashara rasmi tangu soko hiko kuungua.

"Kwa kweli maisha ni magumu dadangu asikwambie mtu, nimejitahidi kukopa pesa, nimenunua mzigo mpaka sasa upo stoo kwa sababu sina eneo la kuuzia, mpaka sasa sielewi ni lini nitapatiwa eneo ili nami niendelee na biashara yangu kama wengine, hali ya maisha ni ngumu bila biashara dadangu asikwambie mtu," alisema.

Akizungumzia malalamiko ya kupewa maeneo yasiyofaa, Katibu wa soko hilo, John Andrew, alisema kikwazo kwa sasa maeneo yamepungua kutokana na kuacha baadhi ya maeneo kupisha njia ya magari kwa hivyo kuna uhaba wa maeneo.

"Tunajitahidi kwa uwezo wetu kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata eneo la kufanyia biashara, hivyo tutakachokipata tunawapatia, sio kwamba tuna maeneo tumeyaficha, hapana, kwa sasa maeneo ni ya shida kwa hiyo waridhike na hicho tunachowapatia," alisema John.

Alisema kukosa eneo kwa machinga wengine kumetokana na wao wenyewe kwa sababu walikataa mchakato wa ugawaji wa vibanda kufanywa upya ili kila mmoja amegewe eneo sawa.

"Baada ya kuturuhusu kuendelea na shughuli zetu katika soko, serikali ilitaka ugawaji wa vibanda uanze upya ili kila mmoja apate, lakini wengi wao walikataa tena kwa kutaka kufanya maandamano na fujo wakitaka kila mmoja arudi alikokuwa mwanzo, sasa hii ndio imeleta huu usumbufu."

Alisema wameshawapatia eneo wafanyabiashara zaidi ya 50 kati ya 200 waliojiandikisha kuwa maeneo yao ya mwanzo waliondolewa kwa ajili ya kuacha eneo litakalotumika kupitia magari na watu kwa urahisi iwapo kutatokea majanga kama haya ya moto.

Hata hivyo alisema kati ya waliojiandikisha kukosa maeneo waligundua kuwa kuna wengine walijichomeka wakati hawakuwa na vibanda katika soko hilo.

"Katika kufanya uchunguzi tulibaini kuwa kati ya hao 200 wengine walijichomeka kutoka maeneo mengine huko ili wapate nafasi hapa na wengine walikuwa na maeneo zaidi ya moja, kwa hiyo tumewachuja na wamebaki takribani 20 tu ndio hawajapata maeneo mpaka sasa na ndio tunapambana kuwatafutia," alisema.

Usiku wa kuamkia Januari 16, 2022 moto uliwaka katika soko la Mchikichini na ulioteketeza sehemu kubwa ya soko hilo lenye wafanyabiashara zaidi ya 3,500, ikiwamo mali zote za wafanyabiashara.

# Faida 6 polisi kuhamia makazi yaliyozuiwa

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limeorodhesha faida sita wanazopata askari wake baada ya kuruhusiwa kuhamia kwenye makazi waliozuiwa kwa miaka mitatu tangu kukamilika kwa ujenzi.

Msemaji wa jeshi hilo, David Misime, ametaja baadhi ya faida hizo kuwa ni nidhamu kambini, uharaka wanapohitajiwa kwenye dharura, usalama kwa askari na kuepuka vishawishi wanavyovipata wakiwa wamepanga mtaani.

Kwa mujibu wa Misime, faida nyingine zinajumuisha kuokoa fedha za serikali kuwakodia makazi na kuwaongezea morali kazini wanapoishi katika mazingira ya kambini.

Kuruhusiwa huko kunatokana na maelekezo ya serikali kuwaruhusu askari kuhamia kwenye majengo hayo yaliyoko Kunduchi mkoani Dar es Salaam miezi kadhaa iliyopita, tangu kukamilika kwake mwaka 2018.

"Hata kile ambacho kilikuwa kinatolewa na serikali kulipa kodi, fedha hizo sasa zitatumika kununua rasilimali zitakazomsaidia askari katika kutekeleza majukumu yake.

"Askari polisi wanapoishi kambini inaongeza nidhamu kwao kwani ni rahisi kuepuka baadhi ya vishawishi.

"Unajua unapompatia askari makazi mazuri, tena katika kambi yenye usalama, inamwongeza morali katika utendaji wao wa kazi," alisema Misime baada ya kuulizwa na Nipashe wiki iliyopita kuhusu tija ya uamuzi huo wa serikali.

Kukwama kwa matumizi ya lengo la mradi huo wa makazi mapya kwa ajili ya askari polisi 330 kulitokana na utata wa hoja ya uhalali wake katika mazingira tajwa, kambi ya polisi.

Mradi huo ulikuwa unahusisha nyumba hizo za makazi ya askari polisi na zile za maofisa wake zilizoko Mikocheni pamoja na kituo kipya cha polisi cha Oysterbay, ambavyo tayari vyote vinatumika.

Ujenzi wa mradi huo ulianza mwaka 2014 na kukamilika mwaka 2018 chini ya usimamizi wa mkandarasi wa Kampuni ya Mara World Tanzania Limited.

Mei 24, mwaka jana, Nipashe ilifanya mahojiano maalum na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, akibainisha sababu za nyumba hizo kutotumika kuwa ni kutokana na mabadiliko ya kisera yaliyofanyika.

Alisema kulikuwa na mkataba kati ya serikali na kampuni iliyojenga nyumba hizo ambazo baadaye sera zikabadilika ikiwa kwamba maeneo ya jeshi yasiingie mikataba na sekta binafsi.

Hata hivyo, alibainisha kuwa wakati huo kulikuwa na majadiliano yaliyokuwa yanaendelea baina ya serikali na mwekezaji ili kupata hatima yake.

Juni 7, mwaka huu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilizuru katika mradi huo na kuridhika nao na kupendekeza askari wahamie huko wakati mambo mengine ya mkataba yakiendelea kufanyiwa kazi.

Juni 19, 2019, aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alizuru kwenye nyumba hizo na kutoa mwezi mmoja kwa Shirika la Rasilimali la Jeshi la Polisi kutoa vielelezo kwa Kamati ya Tathmini iliyoundwa kwa ajili ya mradi wa Ofisi ya Polisi Oysterbay na nyumba hizo ili zikabidhiwe serikalini.

Juni 5, 2016, kupitia taarifa ya vyombo vya habari iliyotolewa na wizara hiyo kupitia kwa Katibu Mkuu wake, Meja Jenerali Projest Rwegasira, Jeshi la Polisi liliagizwa kuwasilisha mkataba wa miradi hiyo baada ya kubainika ni mikubwa na ya muda mrefu.

Miradi hiyo ilitekelezwa kwa gharama ya dola za kimarekani milioni 296 baina ya mwekezaji na serikali.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2019/20, mbali na mambo mengine, ina angalizo kuhusu miradi iliyokamilika lakini haitumiki.

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZA KUTUMIKA KWA MFUMO ULIOBORESHWA WA UWASILISHAJI WA RITANI ZA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)

*Dar es salaam, Alhamis, Februari 03, 2022*

**1.0 Utangulizi**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwatangazia Walipakodi wote waliosajiliwa kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani na Umma kwa ujumla, kuwa imeboresha mfumo wake wa uwasilishaji wa ritani za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Maboresho haya yanalenga kumrahisishia Mlipakodi katika uwasilishaji wa ritani pamoja na ukokotoaji wa Kodi stahiki.

Mfumo ulioboreshwa wa kuwasilisha ritani utaanza kutumika rasmi kuanzia **tarehe 1 Machi 2022** na utatumika katika uwasilishaji wa **ritani za mwezi Machi** ambazo zinatakiwa kuwasilishwa mnamo au kabla ya tarehe **20 Aprili 2022**.

**2.0 Faida Zitokanazo na Mfumo Ulioboreshwa**

Mfumo ulioboreshwa wa kuwasilisha ritani za VAT una faida nyingi kwa watumiaji ikiwa ni pamoja na:-

- Urahisi kwa Mtumiaji ambapo Mlipakodi atahitajika kutumia akaunti moja ya uwasilishaji wa ritani, tofauti na awali ambapo ilimlazimu Mlipakodi kutumia akaunti tofauti kulingana na aina ya ritani ya kodi;
- Ujazaji wa ritani umerahisishwa ambapo taarifa za manunuzi katika ritani ya VAT zitaiingizwa kwa kutumia Namba ya Uthibitisho (Verification Code) tu iliyopo katika risiti ya kielektroniki tofauti na awali ambapo ilimlazimu Mlipakodi kujaza taarifa kadhaa kama Jina la Muuzaji, Namba ya usajili wa VAT, Namba na tarehe ya risiti/Ankara, Kiasi cha manunuzi na VAT katika manunuzi husika;
- Mfumo utawezesha kufanyika kwa marekebisho ya kodi pale yanapotokea kama yalivyoanishwa katika Sheria ya Kodi la Ongezeko la Thamani Sura ya 148 tofauti na utaratibu wa sasa ambapo Mlipakodi alihitajika kuandika barua ya kutoa taarifa kwa Kamishna;
- Mfumo utakokotoa kodi stahiki ya manunuzi wenyewe pale ambapo Mlipakodi atakuwa anajihusisha na bidhaa zinazostahili kulipiwa VAT na zile zilizosamehewa kodi (Partial Exempt Trader); na,
- Mfumo utatoa mrejesho wa upokeaji wa ritani pamoja na makadirio ya kodi mara tu baada ya Mlipakodi kuwasilisha ritani.

**3.0 Namna Mfumo Unavyofanya Kazi na Mambo Muhimu ya Kuzingatiwa**

Mfumo umeboreshwa ili kuweza kuleta ufanisi katika uwasilishaji wa ritani na hivyo kuongeza ulipaji kodi kwa hiari kwa watumiaji. Vitu muhimu vilivyozingatiwa ni pamoja na;

- Mfumo utapatikana katika tovuti ya TRA (www.tra.go.tz) kwa kutumia akaunti ya uwasilishaji wa ritani iliyosajiliwa kuwasilisha ritani za kodi nyingine kama PAYE, SDL, SETPI na ROI;
- **Mfumo utatambua risiti/ankara za EFD zenye namba ya uthibitisho (verification code) tu kwa madai ya kodi ya ongezeko la thamani katika manunuzi. Hivyo, risiti/ankara zote ambazo hazitakuwa na namba ya uthibitisho hazitatambuliwa na mfumo kuanzia ritani za mwezi Machi mwaka 2022;**
- Mfumo utatambua risiti/ankara zenye TIN ya mnunuzi katika madai ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye manunuzi. Hivyo, risiti/ankara zote ambazo hazitakuwa na TIN ya mnunuzi hazitatambuliwa na mfumo kuanzia ritani za mwezi Machi mwaka 2022;
- Mfumo utatambua tu madai ya kodi yatokanayo na malipo ya Ushuru wa Forodha yenye kadhia (TANSAD) halali ya forodha;
- Mfumo utahakiki uhalali wa risiti/ankara na kadhia (TANSAD) ya forodha; na
- Mfumo hautoruhusu kupeleka mbele madai ya kodi ya manunuzi (repayment amount) ambayo yalikuwepo katika mfumo wa awali bali yatatakiwa kuingizwa na TRA baada ya kuhakikiwa.

Ili kuendana na matakwa ya mfumo ulioboreshwa na kuepukana na usumbufu usiokuwa wa lazima, Walipakodi waliosajiliwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

- Walipakodi wote wenye madai ya kodi ya manunuzi (repayment amount) kwenye ritani ya mwezi Februari 2022 watatakiwa kuomba marejesho ya kodi (kwa wale wanaostahili) au kutaarifu ofisi ya TRA husika kuhusu kiasi cha madai ya kodi ya manunuzi (repayment amount) kwa ajili ukaguzi/uhakiki kabla ya kuingizwa kwenye mfumo ulioboreshwa;
- Walipakodi wote wahakikishe wanatumia mashine za EFD za Itifaki 2.1 (Protocol 2.1) ili kutoa risiti/ankara zenye namba ya uthibitisho (verification code).
- Walipakodi waepuke kutumia risiti/ankara au kadhia (TANSAD) ambazo sio halali ili kuepuka hatua za kisheria na usumbufu wakati na baada ya kuwasilisha ritani katika mfumo ulioboreshwa; na
- Mlipakodi atatakiwa kutumia namba ya malipo (Tax Debit Number) iliyopo katika hati ya makadirio (tax assessment) ya kodi iliyotolewa ili kufanya malipo ya kodi husika.

TRA itaendelea kutoa miongozo na mafunzo kwa walipakodi na wadau wengine ili kuwaongezea na kuwajengea uelewa wa kutumia mfumo kwa ufanisi. Aidha, TRA inawasihi walipakodi na wadau wengine kuzingatia na kufuatilia miongozo mbalimbali inayotolewa pamoja na kuhudhuria mafunzo mbalimbali yatakayotolewa kuhusu mfumo huu ulioboreshwa.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

**Tovuti : www.tra.go.tz**
**Namba za Simu bila malipo : 0800 750 075 au 0800 780 078**
**WhatsApp : 0744 23 33 33**
**Barua pepe : huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**A. J. Kidata**
**Kamishna Mkuu**

166904

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi makubwa yanahitajika Simba CAF

**NI** klabu ya Simba pekee kwa sasa inayobeba dhamana ya nchi kwenye michuano ya kimataifa wakati huu Watanzania wakitamani kuona msimu ujao Tanzania inaingiza tena timu nne kwenye michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF); mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Ikumbukwe tayari wawakilishi wengine wa Tanzania Yanga, Azam FC na Biashara United walishaaga michuano hiyo na Simba pekee ndiyo imetinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, ambapo itaanza kurusha karata yake ya kwanza Jumapili wiki hii dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast kwenye mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwa mantiki hiyo, hadi sasa matarajio ya Tanzania kutetea kuingiza tena timu nne msimu ujao, yapo mikononi mwa Simba pekee, na katika hilo hakuna njia ya mkato zaidi ya timu hiyo kufanya maandalizi ya kutosha ili kuweza kufika mbali kwenye michuano hiyo hatua ambayo itaiongezea nchini pointi na kuwa miongoni mwa timu 12 zitakazoingiza timu nne msimu ujao kwenye michuano hiyo ya CAF.

Simba ambayo ipo kundi moja na Asec Mimosas, usgn ya Niger pamoja na RS Berkane ya Morocco, itaanza mechi hizo za hatua ya makundi Jumapili katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Wamorocco hao, huku lengo lao likiwa ni kutinga hatua ya nusu fainali.

Hatuna hofu kwa Simba katika jukumu hilo na malengo yao ya kufika hatua hiyo ya nusu fainali hasa tukizingatia uzoefu wao katika michuano ya kimataifa na ubora wa kikosi chao pamoja na benchi la ufundi.

Jambo la muhimu kwa sasa, ni Simba kujiandaa vema kuelekea mchezo huo ili kuhakikisha inapata ushindi wa kishindo nyumbani kabla ya kwenda kucheza mechi mbili ugenini mfululizo dhidi ya usgn na RS Berkane.

Tunaamini kama Simba itaanza kwa ushindi nyumbani, kutajenga ari kubwa kwa wachezaji kuelekea mechi zinazofuata na hata kwa mashabiki katika kuipa hamasa timu yao, ili kuweza kufikia malengo yao waliojiwekea msimu huu, lakini kupigania nafasi hizo nne kwa Tanzania.

Ikumbukwe nafasi moja inayopambaniwa ya kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF, hadi sasa tayari Libya imefikia pointi za kuingiza timu nne msimu ujao huku ikiwa na timu mbili ambazo bado zipo kwenye michuano hiyo ya CAF, hivyo kama Simba ikishindwa kutinga robo fainali na hata nusu huku zenyewe zikifanya vizuri, ni dhahiri Tanzania itapoteza nafasi ya timu nne msimu ujao.

Hivyo, kinachotakiwa kwa sasa, wakati Simba ikiendelea na maandalizi yake ambayo tunaamini yatakuwa makubwa, Watanzania kwa ujumla tunapaswa kuwa kitu kimoja kwa kuanza kuiombea katika maandalizi yake na hadi siku itakapocheza mechi hiyo nyumbani na zile za ugenini, tukitambua kwamba inalipigania taifa, hivyo kuisapoti mwanzo mwisho.

Tunatamani kuona Watanzania tukiweka pembeni itikadi zetu za kiklabu na kuwa kitu kimoja, na Nipashe tukiwa kama wadau namba moja wa michezo nchini, tunatambua ili kuwa na matarajio makubwa ya timu zetu kufanya vizuri hatuna budi kupigania kuingiza nne kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Nipashe tunatamani kuona Watanzania wote tukiwa kitu kimoja Jumapili kuisapoti Simba hasa kwa kuingiza mashabiki wote 35,000 walioruhusiwa na CAF kuingia uwanjani kipindi hiki ambacho dunia inapambana na janga kubwa la maambukizo ya virusi vya corona.

Hata hivyo, ili CAF kuendelea kuruhusu mashabiki kuingia uwanjani kwa idadi kama hiyo ama zaidi, kila mmoja anapaswa kufuata masharti yalitolewa ya kutakasa mikono kabla ya kuingia uwanjani, kuacha nafasi moja ya kiti uwanjani kwa kukaa kinachofuata na kuvaa barakoa uwanjani hapo.

Lakini kubwa zaidi ni mashabiki sasa kubadili utamaduni wao wakupenda kushangilia pale timu yao inapopata bao ama mchezaji anapopiga chenga na badala yake kushangilia mwanzo mwisho jambo ambalo litawaongezea ari ya kupambana mwanzo mwisho wa mchezo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongereni Tanzanite kwa mlipofikia, haikuwa riziki

Na Adam Fungamwango

**IJUMAA** iliyopita Watanzania walipatwa na huzuni, baada ya timu yao ya Taifa ya Wanawake chini wa miaka 20, maarufu kama Tanzanite ilipochapwa mabao 2-0 mjini Addis Ababa, Ethiopia na timu ya taifa hilo kwenye mchezo wa raundi ya tatu kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia, zinazotarajiwa kufanyika nchini Costa Rica kuanzia Agosti 10 hadi 28, mwaka huu.

Kwa kipigo hicho cha ugenini, Tanzanite imetolewa kwa jumla ya mabao 2-1, kutokana na mechi ya kwanza hapa nchini kushinda kwa bao 1-0.

Ilibaki hatua moja wasichana hao kuingia kwenye vitabu vya kumbukumbu ya soka la Tanzania kwani ingeweza kuiwakilisha nchi kwenye fainali za Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza na ingekuwa ni sifa kwa nchi.

Hata hivyo, ukiangalia timu hiyo ilikotoka hadi ilipofikia kwa ujumla imejitahidi sana na haipaswi kubezwa wala kulaumiwa kwa matokeo hayo.

Kinachotakiwa kwa sasa ni kuwapongeza, na kuwapa moyo kwamba walichokifanya ni sifa kwa taifa, kwani kuna nchi nyingi zimetolewa.

Ikumbukwe kuwa timu hiyo ilianza michuano hiyo kwenye raundi ya pili kwa kucheza dhidi ya Eritrea na kwenda kushinda ugenini mabao 3-0 Septemba na ikashinda mabao 2-0 nyumbani Oktoba mwaka jana. Hii ilikuwa ni raundi ya tatu na hata ukiangalia haijatolewa kwa idadi kubwa ya mabao, badala ni tofauti ya bao moja tu.

Inawezekana kilichowaponza ni kushinda idadi ndogo ya mabao nyumbani. Na hili si tatizo la timu hiyo tu ya wanawake chini ya miaka 20, bali lipo kwa timu zote za Taifa za Tanzania, kuanzia Taifa Stars, ya vijana, hata Wanawake, Twiga Queens.

Kinachotakiwa sasa kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na klabu mbalimbali nchini ni kuandaa vijana wengi zaidi kwa ajili ya siku zinazokuja, kwani walipo inawezekana ikawa ni mwaka wao wa mwisho kucheza michuano hiyo chini ya miaka 20.

Watakwenda kuichezea Twiga Stars na kuongeza kitu huko, lakini tatizo kubwa litakuwa huku chini kupata wachezaji wapya ambao wataibeba tena Tanzania kwenye michuano kama hiyo.

Kuna michuano ya CECAFA, pia Tanzania imekuwa ikialikwa kwenye michuano ya wasichana chini ya miaka 20 kwa Ukanda wa Kusini mwa Afrika (COSAFA) na imekuwa ikifanya vema, pamoja na mashindano mbalimbali ya Afrika.

Klabu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake zinatakiwa wakati huu ambao Tanzanite wametolewa kusaka vipaji vingine, si kwa ajili ya timu zao tu, bali hata kwa timu ya taifa, kwani TFF inategemea kuteua wachezaji kutoka kwenye klabu hizo na si vinginevyo.

Inaeleweka kuwapata wachezaji wa kike ni ngumu sana tofauti na wanaume, lakini wazazi wamekuwa wagumu kuwaruhusu mabinti zao kucheza mchezo huo.

Ila angalau kwa sasa kutokana na maendeleo ya mchezo huo, kuanzishwa kwa Ligi Kuu, kuanza kuonyeshwa mechi za timu za taifa, pamoja michezo ya Ligi ya Wanawake, kumeanza kulegeza kidogo mitazamo ya wazazi na sasa wameona inawezekana kabisa ikawa njia ya mabinti zao kujipatia ajira, kujikwamua kiuchumi na hata kusaidia familia zao.

Mchezaji wa zamani wa Simba, Mussa Hassan Mgosi, wakati akiwa kocha wa Simba Queens, ameshakaririwa akisema kuwa kuna mabinti ambao wameshajenga nyumba, kukarabati nyumba za wazazi wao kutokana na kucheza soka la wanawake.

Hii inaonyesha kuwa angalau soka la wanawake limeshaanza kulipa, hivyo tunategemea kupata vipaji kutoka chini, na inawezekana kabisa Tanzanite mwakani ikapata wachezaji bora zaidi watakaokuja kuungana na walioko ambao hawajazidi umri wa miaka 20 kwa ajili ya kuanza tena harakati za kusaka tena tiketi ya kucheza fainali za mataifa Afrika na pia Kombe la Dunia ambalo ilikuwa almanusura wasichana waipeleke Tanzania nchini Costa Rica.

HABARI KITAIFA

# Wadau wataka polisi washtakiwe

**Na Salome Kitomari**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimependekeza kuboreshwa kwa baadhi ya vifungu kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, ikiwamo vinavyotoa kinga ya kutoshtakiwa kwa polisi wanaofanya operesheni za kificho. Pia kimetaka kufanyika maboresho kwenye kifungu cha kutoweka ukomo wa muda kwa upelelezi.

Kimesema kifungu hicho kimeweka mazingira ya kumkamata na kumweka chini ya ulinzi mtuhumiwa wa makosa makubwa hata kama upelelezi haujakamilika tofauti na masharti yaliyowekwa kwa makosa madogo.

Maofisa uchechemuzi wa LHRC, Raymond Kanegene na William Maduhu, waliwasilisha maoni hayo katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba 7 wa mwaka 2021, ambao umewasilishwa bungeni kwa mara ya pili.

Maduhu alisema kifungu kinachohusu askari wa upelelezi hofu iliyoko ni namna ya kuweza kutenganishwa makosa yatakayoweza kufanywa na maofisa hao ikiwa nje ya operesheni za kificho.

"Kwa kuwa sheria haina kifungu chochote kinaweka mazingira ya kutoa endapo kosa litafanywa nje ya operesheni ya kificho. LHRC ina maoni ya kwamba, mtu yeyote atakayekinzana na sheria kwa makusudi afikishwe katika vyombo vya sheria ili kulinda haki za binadamu," alisema Maduhu.

Kuhusu kutoweka ukomo wa muda kwa mpelelezi, Kanegene alisema makosa yaliyoainishwa ni shambulizi kubwa la mwili, kubaka, uvamizi wa kutumia silaha, usafirishaji haramu wa binadamu, kumiliki silaha, kusafirisha dawa za kulevya, kumiliki kimakosa nyara za serikali na makosa yanayofanana ambayo yanayoweza kusikilizwa na mahakama kuu.

Alisema: "LHRC ina maoni ya kwamba pamoja na uzito wa makosa yaliyotajwa hapo juu, bado kuna haja ya kuwa na ukomo wa muda wa kukamilisha upelelezi kama ilivyo katika nchi ya Uganda siku 120, na Zanzibar miezi sita, ikiwa muda umepita mahakama kuu ina mamlaka ya kumwachia huru mtuhumiwa."

Alisema mambo mazuri yaliyomo kwenye muswada ni kuwekwa kwa zuio la mtu kutokamatwa mara ya pili, ikiwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) akiwasilisha mahakamani taarifa ya kutokuwa na nia ya kuendelea na kesi.

Aidha, Kanegene alisema kifungu kingine kinapendekeza kuweka masharti ya kutomshtaki mtuhumiwa hadi upelelezi utakapokamilika.

"LHRC inaungana na mapendekezo haya kufuatia na ukweli kwamba, kesi zimekuwa zikichukua muda mrefu mahakamani kwa kuahirishwa mara kwa mara kwa sababu ya kutokukamili kwa upelelezi, huku mtuhumiwa akiwa rumande kwa muda mrefu. Hii inaweza kuwa mwarobaini wa changamoto hiyo," alisema.

## Radi yaua, kujeruhi Kilwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKULIMA wa Kitongoji cha Kiukula, Kijiji cha Kiwawa, Kata ya Mandawa, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Jackson Yohana (28), amefariki dunia na watu wengine wanne wamelazwa hospitalini, baada ya kupigwa na radi iliyoambatana na mvua kubwa.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alisema ajali hiyo imetokea Februari 04, mwaka huu, saa 7:30 mchana.

Kitinkwi aliwataja waliolazwa ni Selemani Hamisi Naulugu (28), Selemani Hamisi Mikidadi (27) aliyejeruhiwa mkono wa kulia, Mohamedi Hamisi Naulugu (42) aliyejeruhiwa mdomoni na Saidi Hassani Kibini (50) aliyepata majeraha maeneo ya mgongoni.

Alisema majeruhi hao wamelazwa Hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga) na kueleza hali zao zinaendelea kuimarika.

Pia alisema mwili wa Jackson umehifadhiwa katika Hospitali ya Kinyonga ukisubiri kuchukuliwa na ndugu zake kwa ajili ya mazishi.

Kamanda huyo hata hivyo, alisema mvua hiyo haikuleta madhara zaidi kama kuharibu mali za wananchi.


NMB Karibu yako

Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

### Utoaji wa Hatifungani yenye thamani ya shilingi za Tanzania Bilioni Ishirini na Tano (na ongezeko la shilingi Bilioni Kumi na Tano) kwa kiwango cha riba kisichobadilika hadi mwaka 2025

Benki ya NMB inapenda kutanganza kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) Tanzania kwa kutumia kifungu cha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (Sura ya 79 ya sheria za Tanzania) imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa Benki ya NMB kuhusu Programu ya Utoaji wa Hatifungani ya Muda wa Kati yenye thamani ya jumla ya shilingi za kitanzania billioni 200

Randama ya taarifa kuhusu Hatifungani hii imeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na ipo tayari kusambazwa kwa wawekezaji.

Benki ya NMB ni Mratibu, Benki inayopokea na kulipa, na Msajili. Kampuni ya Orbit Securities Limited ni Dalali Mdhamini. FSD Africa imetoa ushauri kuhusu Muongozo wa Hatifungani zenye Matokeo Chanya kwa Jamii kwa kuzingatia viwango vya Mamlaka ya Kimataifa ya Masoko ya Mitaji (Social Bond Principles 2021); na Sustainlytics imetoa maoni huru kuhusu Hatifungani ya NMB kukidhi matakwa ya Muongozo wa Hatifungani zenye Matokeo Chanya kwa Jamii.

**Taarifa muhimu za dhamana hiyo zinaainishwa hapa chini:**

| | | |
|---|---|---|
| **Mtoaji** | Benki ya NMB | |
| **Maelezo** | Programu ya muda wa kati | |
| **Kiwango cha Programu** | TZS 200,000,000,000 | |
| **Awamu** | 04 | |
| **Maelezo ya Awamu** | Hatifungani ya wateja binafsi na taasisi | |
| **Kiwango cha Awamu** | TZS 25,000,000,000 (na ongezeko la TZS 15,000,000,000) | |
| **Taarifa za Programu** | Hatifungani isiyo na dhamana | |
| **Kiwango cha Chini** | [TZS 500,000 kwa ongezeko la 10,000] | |
| **Muda wa Kuwekeza** | Miaka 3 | |
| **Kiwango cha Riba** | [8.5%] kwa mwaka, itakayolipwa kila baada ya miezi 3 | |
| **Tarehe za kulipa Riba** | [(Machi,Juni,Septemba,Desemba)] kila mwaka mpaka siku ya kuiva | |
| **Kuorodheshwa Soko la Hisa** | Hatifungani itaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, Maombi ya kuorodheshwa yameshapelekwa Soko la Hisa la Dar es Salaam | |
| **Ratiba** | Mauzo yatafunguliwa | Saa 2.00 Asubuhi [Februari 7, 2022] |
| | Mauzo yatafungwa | Saa 11.00 Jioni [Machi 21, 2022] |
| | Ugawaji wa Hatifungani | Saa 4.00 Asubuhi [Machi 24, 2022] |
| | Tarehe ya kuwataarifu wawekezaji (barua pepe/simu) | Saa 8.00 Mchana [Machi 25, 2022] |
| | Tarehe ya Utoaji | Saa 6.00 Mchana [Machi 28, 2022] |
| | Tarehe ya Ukomo | Saa 11.00 Jioni [Machi 28, 2025] |

**MAWASILIANO:**

Nakala za mkataba wa taarifa, bei na fomu za maombi zinapatikana kwenye ofisi zilizoorodheshwa hapa chini na kwenye tovuti ya Benki ambayo ni **www.nmbbank.co.tz**:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Muuzaji** | NMB | Sigifrida Joseph<br>Benki ya NMB | Simu: +255 22 2322037<br>Baruapepe: nmbbond@nmbbank.co.tz. |
| **Benki inayopokea na kulipa** | NMB | Lucky Kyando<br>Benki ya NMB | Simu: +255 22 2322421<br>Baruapepe: nmbbond@nmbbank.co.tz. |
| **Mratibu** | NMB | Gladness Deogratias<br>Benki ya NMB | Simu: +255 22 2322021<br>Baruapepe nmbbond@nmbbank.co.tz. |
| **Mshauri wa Kitaalamu** | fsdafrica | Mary Njuguna<br>FSD Africa | Simu: +254 20 4024000<br>Baruapepe: info@fsdafrica.org. |
| **Maoni ya Taasisi Huru** | SUSTAINALYTICS | Nadia Djinnit<br>Sustainalytics | Simu: (+1) 416 861 0403<br>Baruapepe: nadia.djinnit@sustainalytics.com |
| **Msajili** | NMB | Avith Massawe<br>Benki ya NMB | Simu: +255 22 2322976<br>Baruapepe: nmbbond@nmbbank.co.tz. |
| **Dalali Mdhamini** | | Godfrey Gabriel<br>Kampuni ya Orbit Securities | Simu: +255 22 211 1758<br>Baruapepe: orbit@orbit.co.tz |

www.nmbbank.co.tz



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania PLC, Sitholizwe Mdlalose (kulia), akipata maelezo ya namna wateja wanavyohudumiwa kutoka kwa Meneja Uendeshaji wa Kituo cha Huduma kwa Wateja Vodacom, Jombo Mkono, alipotembelea kituo hicho Mlimani City jijini Dar es Salaam, ili kujitambulisha na kushuhudia mambo mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu watoto kutochanjwa UVIKO-19

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WIZARA ya Afya imetaja sababu ya watoto kutochanjwa chanjo ya UVIKO-19, kuwa inatokana na utafiti kuonyesha hawajaathirika na virusi vya corona kama ilivyo kwa watu wazima.

Ofisa Programu kutoka Wizara ya Afya Mpango wa Taifa wa Chanjo, Lotalis Gadau, alibainisha hayo Ijumaa mkoani Shinyanga, alipoulizwa swali na Nipashe kwanini watoto wadogo hawachanjwi chanjo ya UVIKO-19, kwenye mafunzo ya wanahabari wa Shinyanga na Simiyu ya uhamasishaji chanjo.

Alisema utafiti haujaonyesha kama kuna haja ya watoto wadogo kupatiwa chanjo ya UVIKO-19, kutokana na kamati ya wataalamu ya chanjo bado hawajajiridhisha kupata takwimu za watoto kuathirika na virusi vya corona. "Utafiti unaendelea ili kuona kama watoto wadogo wapatiwe chanjo ya UVIKO-19, ambapo wataalamu wanalifanyia kazi na wakijiridhisha chanjo itaanza kutolewa kwa watoto, mfano nchi ya Sierra Leone wao baada ya kufanya utafiti wanatoa chanjo kwa watoto chini ya miaka 12," alisema Gadau.

Aidha, alitaja chanjo za UVIKO-19 ambazo zimekubaliwa na kerikali kuwa ni Jensen, Sinopharm, Pfizer, Moderna na Sinovac, na kuwataka wananchi ambao wamepatiwa dozi ya kwanza kwa zile chanjo za dozi mbili, warudi kupewa na ya pili ili kukamilisha kinga kamili.

Alitaja pia baadhi ya magonjwa mengine ambayo yapo kwenye mkakati wa kupunguzwa ama kutokomezwa kabisa kwa kutumia chanjo, kuwa ni polio, surua rubela na pepo punda kwa watoto wadogo.

Katika hatua nyingine, alisema mikoa ya Kanda ya Ziwa iko nyuma sana kwenye utoaji chanjo ya UVIKO-19, na kuwataka wanahabari wa mikoa hiyo watumie kalamu zao vizuri ili kuhamasisha wananchi wapate chanjo, ambayo itawalinda wasipate madhara makubwa wakiambukizwa virusi vya corona.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndugile, aliwataja watu ambao wapo kwenye hatari endapo wakiambukizwa virusi vya corona ni vigumu kupona, kuwa ni wale wenye magonjwa nyemelezi wakiwamo wa kisukari, shinikizo la damu, Ukimwi, pumu na athima, na kuwataka wachangamkie kupata chanjo mapema.

Nao baadhi ya wanahabari kutoka Shinyanga na Simiyu, kwa nyakati tofauti waliishukuru Wizara ya Afya kwa kulikumbuka kundi hilo ambalo ni muhimu na kulipatia mafunzo, kuwa wakipata uelewa mpana juu ya chanjo ya UVIKO-19, wataifanya kazi yao vizuri na kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kupata chanjo.

# RPC: Acheni tabia kuhusisha radi na ushirikina

**Na Neema Hussein, KATAVI**

WANANCHI mkoani Katavi wametakiwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), hasa kipindi hiki cha mvua zinazoendelea zikiambatana na upepo mkali pamoja na radi ili kuepusha vifo vitokanavyo na maafa hayo.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani hapa, Ali Hamad, alisema matukio ya radi hayazuiliki isipokuwa watu wachukue tahadhari ikiwamo kuzingatia maelekezo na elimu wanayopewa na wataalamu ikiwamo kutokukaa karibu na miti wakati wa mvua.

Hamad alisema matukio ya radi ni matukio kama matukio mengine wananchi waache kuyahusisha na imani za kishirikina.

"Waache kuamini kuwa kila kinachotokea kimetokea kwa mkono wa mtu, tunajua kuwa haya ni matukio ya asili yanatokana na Mungu mwenyewe," alisema Kamanda Hamad.

Alisema Jeshi la Polisi halitawaacha salama waganga wa kienyeji wanaopiga ramli chonganishi na kuendelea kuchochea migogoro kwa wananchi wakiwaaminisha kuwa matukio hayo yanasababishwa na watu fulani.

Kamanda aliwataka wananchi pamoja na mamlaka husika kufukia mashimo yote yaliyochimbwa kwa ajili ya shughuli za ujenzi na mashimo ya madini ya dhahabu ambayo yanajaa maji kwa kipindi hiki cha mvua na kusababisha vifo kwa watoto wanaocheza karibu na maeneo hayo.

Alisema watoto wanatumbukia kwenye mashimo hayo, lakini maji yanaweza kusababisha hata magonjwa ya milipuko, hivyo amewataka wazazi kuwa waangalifu kwa watoto wao.

# SENAPA yatuliza wananchi upanuzi mipaka

**Na Ambrose Wantaigwa,**
TARIME

HIFADHI ya Taifa ya Serengeti (SENAPA) imewahakikishia wananchi wanaozunguka maeneo hayo upande wa Wilaya ya Tarime kwamba haina mpango wa kupanua mipaka ya ardhi ya hifadhi hiyo.

Mhifadhi Mkuu wa hifadhi hiyo, Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Uhifadhi, Massana Mwishawa, alitoa ufafanuzi mjini Serengeti alipokuwa akijibu hofu hiyo iliyoelezwa na wakazi wa Kijiji cha Karagatonga pembezoni mwa hifadhi hiyo mbele ya mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mwita Waitara.

SENAPA ina barabara katika eneo la ndani ya hifadhi hiyo kwa lengo la kurahisisha shughuli za ulinzi na kuwawezesha wakazi wanaozunguka kufikia makazi na mashamba yao kirahisi.

Wakazi hao katika nyakati tofauti walimweleza mbunge huyo kwamba kwa sasa mamlaka SENAPA wanaendesha zoezi la kulima barabara katika eneo linalotenganisha hifadhi na maeneo ya vijiji bila kuwashirikisha wakihofia upanuzi wa mipaka.

Kwa mujibu wa Kamishna Mwishawa, uamuzi wa kulima barabara katika eneo hilo inatarajia kurahisisha usafiri wa wakulima na wafugaji wa maeneo hayo kufikia mashamba na malisho yao kwa uhakika.

"Uamuzi wa kulima barabara hiyo ulifuata taratibu zote za kuwashirikisha wakazi wanaozunguka hifadhi, na isitoshe itawasaidia wao wenyewe wananchi kufikia mashamba yao kirahisi," alisema Mwishawa.

Mbunge Waitara aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuwa watulivu kwa kuwa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeshatoa maelekezo wananchi wote wanaoishi pembezoni mwa hifadhi wasibughudhiwe hadi hapo itakapotoa maelekezo mengineyo.

"Kwa sasa tunawashauri wananchi wote wanaozunguka hifadhi hiyo kuwa watulivu wakati serikali ikitafuta majibu ya kero zao kwa kuwa Mama Samia (Rais) ameshatoa maelekezo wakazi wote wanaoishi pembezoni mwa hifadhi zote wasisumbuliwe," alisema Waitara.

HABARI KITAIFA

## NBC yawapa neno wafanyabiashara

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC imewataka wafanyabiashara kuendelea kuweka imani kwao hususani kwenye utoaji huduma, huku ikijinasibu kujiwekeza zaidi kwenye sekta ya kilimo na fedha.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Kitengo cha Wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji NBC, James Metaron, kwenye mkutano uliohusisha wawekezaji wakubwa na NBC wakijadili masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

Metaron alisema: "Tunafurahi kuona wateja wetu mnashirikiana na sisi katika huduma mbalimbali kwa takribani miaka 20. Tunawaomba mwendelee kutuamini".

Alisema NBC imejikita zaidi katika kuhudumia wateja wote hususani wakulima kwa kuwawezesha kuwaamini na kupata fedha za kununua mazao kutoka kwa vyama vya ushirika, kuandaa shamba pamoja na utoaji wa biashara.

"Tunatoa huduma za kifedha kwa wateja wakubwa, kwa upande wa kilimo tumekuwa tunawasaidia katika kununua mazao kutoka kwa vyama vya ushirika na hata muda mwingine tunampatia mteja fedha kwa ajili ya kuandaa shamba lake kabla ya kulima," alisema Metaron.

Vilevile alisema NBC imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kilimo kinakua na kupitia NBC na inawahamasisha wateja wadogo na wakubwa kujiunga kutokana na uzoefu mkubwa waliokuwa nao.

"Tunafanya biashara katika sekta zote ila tumejikita zaidi kwenye kilimo ili kusapoti wateja wetu na hata kwa wafanyabiashara wakubwa," alisema Metaron na kuongeza;

"Kwa mwaka 2022 NBC imejizatiti kwa kuwekeza fedha nyingi takribani Sh. bilioni 100 ili kuwasaidia wakulima kununua na kusafirisha mazao ndani na nje ya nchi."

Naye mmiliki wa kampuni ya Woiso inayoshughulika na masuala ya kutengeneza bidhaa asilia za ngozi, Keneth Woiso, alisema akaunti yake ya na NBC ina umri wa kijana.

Alisema katika kipindi chote NBC wamekuwa na msaada mkubwa sana na wameweza kushirikiana vizuri pindi anapokuwa amekwama kwenye masuala ya kibiashara.

**"Tunafanya biashara katika sekta zote ila tumejikita zaidi kwenye kilimo ili kusapoti wateja wetu na hata kwa wafanyabiashara wakubwa," alisema Metaron na kuongeza;**

# Wawarubuni watoto wao wafeli ili walime

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

IMEDAIWA kuwa baadhi ya wazazi katika Kata ya Puni Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wanawashawisha watoto wao kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya mwisho kwa lengo la kuwabakiza nyumbani na kuwasaidia katika shughuli za kilimo.

Hayo yamebainishwa na wajumbe wa kamati za MTAKUWWA ngazi ya kata walipozungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti wakati wa utekelezaji wa mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mmoja wa wajumbe hao, Kinyage Kuyega, alisema wazazi wamekuwa chanzo cha kusababisha watoto wao kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya mwisho ya darasa la saba kwa kuwataka kufanya vibaya ili wabaki nyumbani na kuwasaidia katika shughuli za kilimo na ufugaji.

Naye Saramba Mnkumbi alisema wanafunzi wanapopewa adhabu na walimu shuleni, wazazi wanakuja juu na kuwafokea walimu, hali ambayo inampatia kiburi mwanafunzi na hata kama shuleni alikuwa na uwezo mkubwa kwenye mtihani wa mwisho atafanya vibaya na mzazi hashtuki.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Puni, Leonard Kawili, alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 582 kati ya hao wanafunzi wa kike ni 297 na wakiume 285, na kwamba wanafunzi walioacha shule bila kutambua sababu ni nini, ni saba pekee na walikuwa wanafanya vema darasani.

"Kuna mwanafunzi kati ya wanafunzi saba walioacha masomo na alikuwa anafanya vema darasa, tulijitahidi kumrejesha shuleni kwa kushirikiana na mzazi wake, lakini majibu aliyotujibu yalikuwa hayaendani na umri wake...tulikuja kubaini alikuwa ameharibika na uvutaji wa bangi, hivyo aliacha shule," alisema Kawili.

Ofisa Kilimo wa kata hiyo, Samwel Mayala, alithibitisha kuwapo kwa baadhi ya wazazi ambao wamekuwa na tabia ya kuwazuia watoto wao kwenda shuleni na kubaki nyumbani kulea wadogo zao na wengine kuelekea kwenye shughuli ya uchungaji wa mifugo siku za masomo.

Alisema amekuwa akipokea orodha ya wanafunzi watoro kutoka shule za msingi na sekondari kupitia ofisi ya mtendaji wa kata yake na hivi karibuni alipokea orodha ya wanafunzi 85 na baada ya kufuatilia wengi walidai wanazuiliwa na wazazi wao kuendelea na masomo.

"Katika kijiji cha Nyashimbi nilikuta mwanafunzi wa darasa la tano anachunga mifugo ya jirani wakati wa masomo, baada ya kumhoji alidai mama yake amemzuia kwenda shule akachunge mifugo ya jirani ili wapate fedha za mahitaji ya familia," aliongeza Mayala.

Aliwataka wazazi kuachana na mila potofu ya kuwazuia watoto wao kuendelea na masomo na badala yake wahakikishe wanahudhuria masomo wakati wote na kwa mzazi ambaye atabainika kuwa na mwanafunzi nyumbani, atawajibishwa kisheria ili kuondoa urasimu unaowanyima watoto haki ya kusoma.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (kulia waliokaa) na Rais wa Mastercard Kanda ya Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, Mark Elliot (kushoto) wakitia saini makubaliano ya ushirikiano wa miaka 5, ili kuendeleza ubunifu kupitia njia ya malipo ya kidijitali nchini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi mitaa wapewa jukumu urasimishaji ardhi

**Na Salome Mwasamale**

DIWANI wa Kata ya Mbezi, mkoani Dar es Salaam, Ismail Malata, amewataka viongozi wa serikali za mitaa kushirikiana na kamati za urasimishaji ardhi na kampuni za upimaji katika kuainisha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma za kijamii.

Lengo ni kuyafikisha katika vikao vya Baraza la Madiwani kwa ajili ya fidia kuondoa changamoto ya uvamizi.

Malata alitoa rai hiyo kwenye kikao kazi cha tathmini ya namna ya kutatua changamoto mbalimbali zikiwamo za migogoro ya ardhi inayojitokeza katika zoezi la urasimishaji ardhi linaloendelea katika Kata ya Mbezi.

Alisema mpango wa urasimishaji ardhi hautoi haki ya mwananchi katika kumiliki ardhi badala yake wanapaswa kushirikishwa katika zoezi la utoaji ardhi kwa ajili ya huduma za jamii na kulipwa fidia zao inapobidi.

"Ardhi ni haki ya mtu, hivyo viongozi mnapaswa kushirikiana sambamba na kuwashirikisha wananchi katika suala la utoaji ardhi kwa ajili ya huduma za jamii ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima na kulipa fidia kwa wanaohitaji fidia," alisema.

Jitihada za ziada zinahitajika hasa katika maeneo yanayoendelea kuhakikisha yanatengwa maeneo kwa ajili ya huduma za jamii ili kuepuka hasara ya uvunjaji wa maeneo katika siku za usoni.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mkurugenzi wa Kampuni ya Geo Plan, Leonard Bamuisa, ambaye anapima mitaa mitatu ya Mbezi Makabe, Msumi na Mpiji Magohe, alisema changamoto kubwa wanazokutana nazo na kukwamisha zoezi hilo lisikamilike kwa wakati kuwa ni pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kuwacheleweshea wananchi waliokamilisha hatua zote za upimaji hundi ya malipo (control number) kwa ajili ya upatikanaji wa hati.

Bamuisa aliitaja changamoto nyingine ni ucheleweshwaji wa serikali katika kuyafuta mashamba ya awali ili upimaji uendelee na ile ya wananchi kuchelewesha malipo ya gharama za upimaji kwa kampuni za urasimishaji ardhi.

"Kampuni zinapata kero kubwa kutoka kwa wale wachache ambao wameshafanya malipo ya urasimishaji ardhi kwa kuwa wanahitaji kupata hati, lakini haiwezekani kwa kuwa kuna upimaji wa mashamba ya awali ili wapate lazima upimaji wa mashamba ya awali ufutwe ili vipimwe viwanja," alisema.

# Waganga wa kienyeji wazua balaa

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAKAZI wa Kata ya Puni Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wameiomba serikali kusajili waganga wa jadi walioko katika kata yao, ili kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyofanywa na wanawake wanaokwenda kwa waganga hao kuwaroga waume zao ili wawapende.

Hayo waliyabainisha juzi wakati wakizungumza na Nipashe lililofika kijijini hapo ili kutambua mila na desturi zinavyochangia ukatili wa kijinsia chini ya mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mradi huo unatekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga (SPC) kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mmoja wa wakazi hao, Amosi Daudi, alisema wanawake wamekuwa wakiwafanyia waume zao vitendo vya kikatili kwa kuwaendea kwa waganga wa jadi na kuwaroga ili wawapende hali ambayo imekuwa ikisababisha wanaume ndani ya familia kuteswa na wake zao.

Alisema vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa na waganga wa jadi ambao wamekuwa wakiwalaghai wanawake kuwa wana dawa za kuwatulia waume zao jambo ambalo si kweli.

Naye Abdallah Magoko alisema kuna waganga huko vijijini wamekuwa wakipiga ramli chonganishi kwa kuwachonganisha wananchi na wakati mwingine wanajihusisha katika vitendo vya mapenzi na wanawake wanaofika kupata huduma na kuiomba serikali kuingilia katika jambo hilo.

Kwa upande wake, Mtendaji wa Kata ya Puni, Fumbuka Mathias, alisema wamekuwa wakiendesha msako wa mara kwa mara kwa waganga wa jadi wasiokuwa na vibali na wakiwabaini wanawashauri kwenda halmashauri kujisajili ili kuendesha shughuli zao katika hali ya usalama. Aidha, alisema awali kulikuwa na waganga wengi waliokuwa wakiendesha shughuli zao bila usajili na lilipotokea tatizo walijitokeza kuomba msaada ndani ya serikali.

Sera ya afya ya mwaka 2007 inaweka bayana kwamba serikali itashirikiana na watoa tiba mbadala wakiwa na vibali maalumu katika kutoa huduma na siyo kuendesha shughuli zao kinyume cha utaratibu.




Msimamizi wa Programu kutoka Kitengo cha Habari cha Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Jackson Malangalila, akizungumza kwenye Semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), Serikali ya Mtaa wa Amani, Kipunguni, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukeketaji. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Teknolojia mtandao yasajili kesi 551 Lindi

**Na Said Hamdani,** LINDI

UJIO wa teknolojia mpya ya mawasiliano nchini, umewezesha kusajili kesi 551 mkoani Lindi kati ya jumla ya mashauri 3,767 yaliyofunguliwa mkoani humo.

Mashauri hayo yamefunguliwa katika mahakama mbalimbali za Mkoa wa Lindi, huku 551 zikisajiliwa kupitia njia ya mtandao kwa kipindi cha miezi 13 iliyopita. Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi Mahakama ya Mkoa wa Lindi, Consolata Singano, alibainisha hayo katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini, ambayo kimkoa yalifanyika viwanja vya Mahakama ya Mkoa.

Singano alisema mashauri 551 yamesajiliwa kwa njia ya mtandao kwa wilaya zote tano za Mkoa wa Lindi za Kilwa, Nachingwea, Liwale na Ruangwa, mwaka 2021 na Januari mwaka huu.

Alisema mashauri 479 kati ya 551 yaliyofunguliwa kwa njia ya mtandao mwaka 2021 na 72 yalisajiliwa Januari 2022 na kufanya idadi ya kesi na mashauri yalisajiliwa kwa njia ya Mtandao mkoani Lindi kufikia 551.

Singano ameeleza kwamba kesi 72 zilizosajiliwa Januari mwaka huu Wilaya ya Kilwa ilisajili 24 ikifuatiwa Nachingwea (17), Liwale (16), Lindi (08), Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi Mkoa (05) na Ruangwa (02).

Alisema mfumo huo unatumika kwa mahakama za Wilaya na Mkoa pekee, wakati za mwanzo zinaendelea kutumia mfumo wa zamani.

"Ikumbukwe mahakama za mwanzo bado zinaendelea kutumia mfumo tofauti kidogo na ule za wilaya na mkoa," alisema Singano.

Hakimu Singano alisema Mahakama imeweka mkakati kuwawezesha wananchi na wateja wao, wanapata na kujulishwa taarifa za mwendo wa mashauri yao kupitia njia ya ujumbe mfupi wa simu zao za mkononi na barua pepe.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, ambaye alikuwa mgeni rasmi aliwataka wananchi kujenga tabia ya kujitokeza kwenda mahakamani kutoa ushahidi wanapohitajika, kuwawezesha mahakimu kutekeleza majukumu yao ya utoaji haki.

Ndemanga alisema kutokana na baadhi ya wananchi kujenga tabia ya kutojitokeza mahakamani wanapohitajika, hasa kwa kesi zinazohusu mimba kwa wanafunzi wa kike, hutoa nafasi wahalifu kuwachiwa huru kunakochangiwa kukosekana kwa ushahidi, ambao ungesaidia wahusika kupewa haki zao.

## Rais MasterCard Afrika ashuhudia droo ya 5 NMB MastaBata

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mpya wa MasterCard International Kanda ya Afrika, Mark Elliott, ameshuhudia droo ya wiki ya tano ya Kampeni ya NMB MastaBata, ambako washindi 100 wamejishindia jumla ya Sh. milioni 10, hivyo kufanya pesa zilizotolewa kwa washindi 525 kufikia Sh. milioni 75 Kati ya zaidi ya Sh. milioni 200 zinazoshindaniwa.

NMB MastaBata - Kivyako Vyako,' ilianza mwishoni mwa Desemba 2021, ambako kila wiki washindi 100 hutafutwa kupitia droo zinazosimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT). Washindi 25 wa droo ya mwisho wa mwezi hujishindia Sh. milioni 1 kila mmoja, huku wana fainali 30 wakitarajiwa kujinyakulia Sh. milioni 3 kila mmoja Machi mwishoni.

Kampeni hiyo ya wiki 10, inahamasisha matumizi ya kadi za MasterCard, Masterpass QR na Vituo vya Mauzo (PoS), ambako tayari washindi 525 Kati ya 1,080 wamejinyakulia Sh. milini 75 kati ya zaidi ya Sh. milioni 200 zinazoshindaniwa. MasterCard ni washirika wa kibiashara wa NMB, ambako mwaka jana 2021 Kampuni hiyo iliitunukia NMB Tuzo ya Benki Kinara Katika Kuhamasisha Matumizi ya Kadi, ambako Rais Mark Elliott, alishuhudia moja ya droo za kampeni mbalimbali za kuhamasisha matumizi hayo yasiyohusisha pesa taslimu.


Rais Elliot ambaye ni mpya madarakani, Alhamisi alitembelea NMB kujionea huduma mbalimbali na shughuli za kiutendaji na kiuendeshaji kwa jumla, ambako amekiri kuvutiwa na Kampeni ya MastaBata na huduma za benki hiyo kwa ujumla.

Meneja wa Idara ya Kadi NMB, Sophia Mwamwitwa, alisema tayari washindi 400 wa droo za kila wiki walishatwaa Sh. milioni 40, huku washindi 25 wa droo ya mwisho wa mwezi Januari wakijinyakulia Sh. milioni 25, hivyo kupatikana kwa washindi 100 wa droo ya 5, kuigawa kampeni hiyo nusu kwa nusu kuelekea 'Grande Finale' mwishoni mwa Machi mwaka huu.

"Tayari washindi 400 wamenufaika na Sh. 100,000 kila mmoja kwa droo za mwisho wa wiki, sambamba na washindi 25 wa Januari waliojinyakulia Sh. milioni 1 kila mmoja. Tuko katikati ya kampeni yetu, kwani tumebakisha wiki 5, droo moja ya mwisho wa mwezi Februari, pamoja na fainali mwishoni mwa kampeni hii.

"Wito kwa Watanzania ni kuchangamkia fursa za kujishindia motisha hizi. Wenye akaunti waendelee kutumia kadi zao kufanya miamala, malipo na manunuzi, na wale wasio na akaunti, wajitokeze matawini kufungua na kuomba kadi, ili kukidhi kigezo kikuu cha ushiriki wa kampeni hizi na kunufaika na zawadi za pesa taslimu," alisisitiza Mwamwitwa.

Nipashe Spotika




WACHEZAJI 10 WANAOLIPWA KUPITA UWEZO WAO UWANJANI UK. 12




Pierre-Emerick Aubameyang (kulia), akitambulishwa rasmi Barca baada ya kusajiliwa katika dirisha la Januari.
**PICHA: MTANDAO**

# KLABU 5 ZILIZOTUMIA FEDHA NYINGI JANUARI

**LONDON, England**

TUKO zaidi ya nusu ya msimu wa sasa wa ligi za soka za Ulaya. Dirisha dogo la usajili la Januari limeshuhudia klabu kadhaa kubwa zikisajili wachezaji wapya kwa ajili ya kujiimarisha.

Ingawa uhamisho wa hali ya juu kwa kawaida hufanywa wakati wa majira ya joto, dirisha la Januari hutoa njia kwa klabu kuboresha timu zao katikati ya msimu. Usajili wa msimu wa baridi mara nyingi umeonekana kuwa baraka kwa klabu.

Hebu sasa tuangalie timu tano ambazo zimetumia fedha nyingi zaidi katika dirisha la usajili la Januari...

**#5. Everton: Euro Mil. 38**

Mazingira pale Goodison Park yamekuwa si ya kuvutia sana. Everton imekuwa ikijitahidi kupata ushindi, lakini imekuwa na matatizo nje ya uwanja pia. Rafa Benitez hakuweza kufanya uchawi wake na alifutwa kazi baada ya miezi sita tu ya kuinoa klabu hiyo.

Walitumia Euro milioni 38 Januari na wameleta mabeki wawili wa pembeni ili kuimarisha safu yao ya ulinzi. Usajili wa kwanza wa klabu hiyo ulikuwa wa Nathan Patterson kutoka Rangers. Everton walilipa euro milioni 15 pamoja na nyongeza kwa beki wa kulia. Beki wa kushoto wa Dynamo Kyiv, Vitaliy Mykolenko, ndiye aliyefuata, ambaye ada ya takriban Euro milioni 21 ililipwa.

Everton wameshinda mechi tano pekee za Ligi Kuu England msimu huu na wako nafasi ya 16 kwenye ligi. Hali yao ya hivi majuzi imekuwa mbaya, na Frank Lampard ameteuliwa kuchukua jukumu la kuiongoza.

**#4. Liverpool: Euro Mil. 45**

Ingawa wengi walitarajia Liverpool kuwa na kipindi tulivu cha Desemba-Januari, klabu hiyo imeonyesha ulimwengu kile wanachoweza ndani na nje ya uwanja wa soka. Biashara yao ya uhamisho imeonyesha kuwa wamiliki FSG wamejitolea kusaidia klabu kupigania mataji.

Liverpool wametumia Euro milioni 45 kwenye dirisha la usajili la Januari. Wamemleta Luis Diaz wa Porto baada ya kupambana na Tottenham Hotspur. Mchezaji huyo wa Colombia mwenye umri wa miaka 25, ni mfungaji mabao hodari na atakuwa nyenzo ya thamani kwa kikosi cha kocha, Jurgen Klopp. Amefunga mabao 14 na kutoa asisti tano katika mechi 18.

Liverpool kwa sasa wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi na wanaweza kupunguza pengo la Manchester City hadi pointi sita pekee iwapo watashinda mchezo wao wa mkononi. Wengi walitarajia 'Wekundu' hao kuporomoka bila uwapo wa Sadio Mane na Mo Salah, lakini wameweza kusimamia hali hiyo kwa kiasi kikubwa.

**#3. Barcelona: Euro Mil. 55**

Barcelona imekuwa katika msukosuko tangu mwaka jana. Pamoja na kuondoka kwa Lionel Messi wamekuwa na matatizo ya kifedha pia. 'Blaugrana' hao wametumia jumla ya Euro milioni 55 katika dirisha la usajili la Januari.

Usajili wa kwanza wa Barcelona kwenye dirisha la Januari alikuwa Ferran Torres. Barcelona ililipa Manchester City ada ya takriban Euro milioni 55 kwa winga huyo. Pia wamemsajili winga wa Wolves, Adama Traore na Pierre-Emerick Aubameyang kutoka Arsenal.

Barcelona wako katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa La Liga, pointi 15 nyuma ya vinara na wapinzani wao, Real Madrid. Watamenyana na Napoli kwenye Ligi ya Europa. Michuano hii inaweza kuwa njia pekee ya Barca kuokoa kile ambacho kimekuwa janga la msimu.

**#2. Juventus: Euro Mil. 82**

Ingawa Juventus wanaweza kuwa na wakati mgumu kwenye Serie A msimu huu, biashara yao ya uhamisho wa majira ya baridi bila shaka itakuwa imeweka tabasamu kwenye nyuso za mashabiki wao. Juventus wametumia jumla ya Euro milioni 82 katika dirisha la uhamisho la Januari. Wachezaji wao waliosajiliwa hivi karibuni ni Federico Gatti kutoka Frosinone ya Serie B na Denis Zakaria kutoka Borussia Monchengladbach.

Usajili wao mkubwa, hata hivyo, umekuwa ule wa Dusan Vlahovic. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, yuko katika hali mbaya na alikuwa anatakiwa na klabu kadhaa maarufu barani Ulaya. Juve walilipa Euro milioni 70 kwa mshambuliaji huyo wa Serbia.

Kampeni ya Juventus ilianza kwa njia mbaya sana na ilikuwa moja ya ligi mbaya zaidi kuanza kwa karibu miaka 50. Wanaonekana kuwa wametulia hivi karibuni, lakini nafasi yao ya kutwaa ubingwa wa ligi ni ndogo sana. Mashabiki wa Juve watakuwa na matumaini kwamba kwa wachezaji hao wapya waliosajiliwa, Bianconeri wanaweza kumaliza msimu kwa kasi.

**#1. Newcastle United: Euro Mil. 87**


Newcastle ilinunuliwa Oktoba 2021 na mashabiki wamekuwa na wasiwasi tangu wakati huo. Klabu ilikuwa na msimu mbaya, na bodi hatimaye ikalazimika kubadili kocha mkuu. Eddie Howe alichukua nafasi ya Steve Bruce Novemba mwaka jana.

Howe atafurahishwa na bajeti mpya ya uhamisho aliyonayo. Newcastle wametumia jumla ya Euro milioni 87 kwenye dirisha la usajili la majira ya baridi. Chris Wood wa Burnley, Kieran Trippier wa Atletico Madrid, na Bruno Guimaraes wa Lyon wote wamejiunga na 'Magpies' hao. Dili la Guimaraes lilikuwa ghali zaidi, huku Newcastle wakilipa ada ya karibu euro milioni 50 kwa Mbrazili huyo.

Kwa sasa Newcastle wako nafasi ya 18 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, lakini wanaweza kutoka kwenye eneo la kushushwa daraja iwapo watashinda mchezo wao mkononi. Kwa usajili walioufanya, Magpies wanapaswa kumaliza msimu wakiwa juu.

## ISIKUPITE

SERGIO Aguero ndiye mchezaji anayeongoza kwa kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa mechi kwenye Ligi Kuu England (akiibeba mara saba) katika kipindi chake akicheza kwenye ligi hiyo, kuanzia mwaka 2015 hadi 2017, anafuatiwa na Steven Gerrard (mara sita), Harry Kane (mara sita), Cristiano Ronaldo (mara tano) na Wayne Rooney mara tano.



# WACHEZAJI 10 WANAOLIPWA KUPITA UWEZO WAO UWANJANI




**LONDON, England**

MPIRA wa miguu ni mojawapo ya michezo inayoleta faida kubwa duniani kote, ambapo mabilioni ya pauni huwekezwa katika mchezo huo kila mwaka. Klabu hutumia asilimia kubwa ya fedha hizo kulipa mishahara ya wachezaji wao.

Klabu zinawapa wachezaji mikataba na kuwalipa kulingana na matokeo wanayotarajia, lakini si kila mchezaji anaweza kufikia kiwango bora baada ya kupokea kiasi kikubwa cha fedha. Mara nyingi, mishahara hii ya wachezaji inaweza hatimaye kuwa shida, kama ilivyo kwa FC Barcelona mwaka 2021, na klabu hulazimika kuwauza wachezaji.

Klabu nyingine zina bili za mishahara zinazofikia mamia ya mamilioni ya pauni kila mwaka, na ni kawaida tu kwa idadi nzuri ya wachezaji kulipwa kupita kiasi.

Makala haya inawaangalia nyota 10 wa soka wanaolipwa kupita kiasi duniani kwa sasa kulingana na data kutoka Spotrac.com.

**#10. Kepa Arrizabalaga (Pauni 155,000)**

Kepa Arrizabalaga alijiunga na Chelsea kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia mwaka 2018 na kutia saini mkataba wa miaka saba ambao ulimwezesha kupokea nyongeza kubwa ya mshahara wake. Raia huyo wa Hispania hupokea pauni 155,000 kwa wiki, na hivyo kumfanya kuwa miongoni mwa makipa wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani. Uchezaji wa Kepa, hata hivyo, haujahalalisha ujira wake huo mkubwa.

Kepa itakuwa ngumu kuuzwa kutokana na majaribio ya Chelsea kutaka kurejesha fedha nyingi walizomlipa, huku hata mshahara wake ukiwa kikwazo kununuliwa na timu nyingine, kwani alipata ofa ya mkopo pekee kutoka Valencia na Sevilla.

Baada ya msimu wao wa kwanza wa kuvutia, kipa huyo alianza kufanya vibaya. Hivyo, Chelsea ililazimika kusajili golikipa mwingine, Edouard Mendy, ambaye amecheza nafasi ya nyota huyo tangu wakati huo na kuifanya jezi nambari moja kuwa yake. Kepa hajacheza kwa kiwango kinachotarajiwa pale Chelsea licha ya mshahara wake kuwa mkubwa.

**#9. Callum Hudson-Odoi (Pauni 180,000)**

Winga wa England, Callum Hudson-Odoi alisifiwa kama kipaji kizuri kinachochipukia baada ya kuingia katika akademi ya Chelsea, kiasi kwamba Bayern Munich walimtaka kwa udi na uvumba. Kutokana na hali hiyo, Chelsea walimkabidhi mkataba mpya unaoaminika kuwa na thamani ya mshahara wa hadi pauni 180,000 kila wiki pamoja na bonasi.

Winga huyo ameshindwa kufikia kilele ambacho kilizifanya Chelsea na Bayern kumenyana ili kupata dili la kumnunua. Ameifungia Chelsea mabao manne pekee ya ligi tangu mwaka 2018.

**#8. Timo Werner (Pauni 272,000)**

Mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner alijiunga na Chelsea kwa nia ya kwenda kumaliza matatizo yao ya ufungaji mabao, lakini kwa kiasi kikubwa ameshindwa katika suala hilo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika klabu hiyo akiwa na mshahara wa pauni 272,000 lakini ameshindwa kuonyesha kiwango cha juu.

Mshambuliaji huyo wa Ujerumani, katika mahojiano ya hivi majuzi, alikiri kwamba hajacheza katika kiwango kinachohitajika katika klabu hiyo. Werner amefunga mabao saba pekee ya Ligi Kuu.

**#7. Jadon Sancho (Pauni 350,000)**

Baada ya kushindwa kufanya vema kwenye michuano ya Europa katika majira ya joto, Jadon Sancho alijiunga na Manchester United kwa takriban pauni milioni 73, na hivyo kumaliza uvumi juu ya mustakabali wake. Winga huyo mchanga alipamba vichwa vya habari wakati akitamba kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa na Borussia Dortmund na Manchester United ilikuwa inamwania tangu mwaka 2018.

Baada ya kujiunga na 'Mashetani Wekundu' hao, Sancho alisaini mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya kulipwa pauni 350,000 kwa wiki, lakini ameshindwa kutamba. Mchanganyiko wa hali mbaya na masuala ya kujiamini yamemfanya Muingereza huyo mchanga kuwa na mchango mdogo sana kwa Man United.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao mawili pekee katika mechi 23 katika mashindano yote.

**#6. Anthony Martial (Pauni 250,000)**

Anthony Martial na Manchester United walikuwa wakizozana kabla ya kujiunga kwa mkopo kule Sevilla. Mshahara wa Martial umethibitika kuwa kikwazo kwa klabu kumsajili moja kwa moja, kwani anapokea takriban pauni 250,000 kila wiki.

Mshambuliaji huyo alijiunga na Man United akiwa kijana kutoka AS Monaco, lakini hajawa na mchango mkubwa sana.

**#5. Philippe Coutinho (Pauni 380,000)**

Kiungo wa kati wa Brazil, Philippe Coutinho hivi majuzi tu alijiunga na Aston Villa kwa mkopo na chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu mwishoni mwa msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alivumilia kipindi kibaya sana katika klabu ya Barcelona kabla ya kurejea Ligi Kuu England.

Coutinho alijiunga na wababe hao wa Hispania kwa kitita cha pauni milioni 115 akitokea Liverpool, lakini alitatizika kufanya vema katika klabu hiyo. Mkataba wa Coutinho huko Nou Camp unajumuisha malipo ya pauni 380,000 kwa wiki, jambo ambalo linawakera mashabiki wa klabu hiyo.

Coutinho alifunga mabao 25 katika mechi 106 alizochezea Barcelona kabla ya kuhamishiwa Aston Villa, ambako anatarajia kufufua soka lake.

**#4. Eden Hazard (Pauni 416,000)**

Wakati mwingine, ndoto zinaweza kuwa mbaya. Eden Hazard aliondoka Chelsea na kuelekea Real Madrid mwaka 2019 ili kutimiza ndoto yake ya utotoni, na amekumbana na matatizo mengi tangu wakati huo. Mshambulizi huyo mahiri alijiunga na Los Blancos hao kwa zaidi ya pauni milioni 100 na kusaini mkataba ambao ungemfanya kupokea mara mbili ya kile alichokuwa akipata kule Chelsea.

Majeraha yamemfanya nahodha huyo wa Ubelgiji kutoichezea Real Madrid mara kwa mara na kumfanya acheze mechi 59 pekee. Hazard anapokea kiasi cha pauni 416,000 kila wiki, lakini ameshindwa kuhalalisha mshahara huo mkubwa miaka mitatu ndani ya mkataba wake klabuni hapo.

**#3. Oscar (Pauni 540,000)**

Kiungo wa zamani wa Brazil, Oscar alikuwa nyota wa 'Selecao' kwenye Olimpiki ya mwaka 2012 na alisajiliwa na Chelsea. Oscar alikaa kwa misimu mitano pale Stamford Bridge kabla ya kukamilisha uhamisho wa kushtukiza kwenda klabu inayoshiriki Ligi Kuu ya China, Shanghai SIPG.

Wakati fulani baada ya uhamisho wake kwenda China, kiungo huyo aliulizwa maswali na waandishi wa habari kuhusu nia yake ya kurejea Ulaya. Jibu la Oscar lilikuwa kwamba uamuzi wake wa kusalia nchini China ulichangiwa na kiasi kikubwa cha fedha alichokuwa akilipwa.

Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 30, kwa sasa anapokea takriban pauni 540,000 kwa wiki. Amekuwa akihusishwa na kuhamia Barcelona wiki za hivi karibuni kama mbadala wa Philippe Coutinho aliyeondoka.

**#2. Aaron Ramsey (Pauni 400,000)**

Tangu aondoke Arsenal kwenda Juventus kwa uhamisho wa bila malipo, Aaron Ramsey amekuwa na wakati mgumu katika kupata kiwango na kujiamini kule Turin. Mchezaji huyo wa Wales kwa sasa anapokea kiasi cha pauni 400,000 kila wiki na amejiunga kwa mkopo na klabu ya Rngers ya nchini Scotland.

Ramsey ameichezea Juventus mara 70 tangu alipohamia hapo mwaka 2019, akifunga mabao sita na kutoa pasi za mabao sita. Kocha wa Juventus, Massimiliano Allegri hakumung'unya maneno aliposema anatumaini kumhamisha Ramsey katika dirisha dogo la usajili lililopita na alifanya hivyo.

**#1. Gareth Bale (Pauni 508,000)**

Winga wa Real Madrid, Gareth Bale amewachezea Los Blancos hao mara tatu pekee msimu huu na kuifungia bao moja. Nahodha huyo wa Wales alijiunga na Real Madrid kutoka Tottenham Hotspur kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia ya pauni milioni 86 mwaka 2013.

Bale amekuwa na mzozo na Real Madrid kwa miaka michache iliyopita baada ya maoni yake alipokuwa kwenye majukumu ya kimataifa na Wales. Kocha wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane alijaribu kumfanya winga huyo aondoke pale Santiago Bernabeu kwa kutompa nafasi ya kucheza, lakini Bale alibaki klabuni hapo. Winga huyo alikwenda Tottenham kwa mkopo kabla ya kurejea Real Madrid baada ya kumalizika kwa mkataba wake wa mkopo.


Bale alikaribia kuondoka na kwenda kwenye Ligi Kuu ya China mwaka 2020, lakini dili hilo lilizuiwa na Real Madrid dakika ya mwisho. Bale hajaichezea Real Madrid katika misimu ya hivi karibuni, na bado anapokea kiasi cha pauni 508,000 kila wiki, na kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo.

## Nukuu

"Wavulana hawa wawili ni wapiganaji wa kweli. Wako tayari kila wakati. Wote wawili hawana wasiwasi kuhusu likizo, kuhusu siku za kupumzika na mambo kama haya. Sikuwahi kuwasikia wakiuliza chochote kuhusu kuwa na wakati wa mapumziko. Sikuwahi kufanya. Hasa kwa wavulana hawa wawili ni rahisi sana," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akiwamwagia sifa wachezaji wa klabu hiyo, Mohamed Salah na Sadio Mane saa chache kabla ya mechi yao ya fainali ya AFCON nchini Cameron jana kati ya Misri na Ivory Coast.**



"Kuwa na [Erling] Haaland na [Kylian] Mbappe itakuwa nzuri kwa La Liga na soka kwa ujumla. Lakini kama ningelazimika kuweka bashiri, ningesema kwamba hawatacheza katika timu moja. Ikiwa watahama kutoka kwa klabu zao sasa, hata hivyo kama ningekuwa Haaland na ninataka kushinda Ballon d'Or, nisingeenda kwenye timu moja na Mbappé," **Beki wa Barcelona, Gerard Pique.**



"Matarajio yangu bado ni yale yale. Nataka kushinda mataji na klabu. Hilo litakuwa akilini mwangu hadi siku ya mwisho nitakapokuwa klabuni hapa. Sijui itakuwa lini, lakini hadi hapo ninaamini kuwa naweza kushinda mataji nikiwa na klabu hii kwa sababu nadhani tunaweza na nadhani klabu inastahili, mashabiki wanastahili na pia wachezaji tunastahili kushinda kombe. Wakati wowote, tunapaswa kufanya hatua kwa hatua na kuelewa tuna sifa hizo lakini tunapaswa kuelewa jinsi ya kufanya hivyo, jinsi ya kuweka kila kitu pamoja - ubora na nguvu na kila kitu," **Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes akiamini wanaweza kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ama Kombe la FA.**



# MAKINDA 6 TISHIO LIGI KUU TANZANIA BARA



Peter Banda

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kumekuwa na wachezaji wengi vijana kutokana ndani na nje ya nchi.

Na hawapo tu mradi kujaza nafasi ya wachezaji 25 au 30 wanaoruhusiwa kusajiliwa, la hasha, badala yake kwa namna moja ama nyingine wamekuwa wakizisaidia timu zao zinazopambana kwenye ligi hiyo.

Ilikuwa ni mara chache sana kuona wachezaji vijana, hasa kwenye timu kubwa za Simba, Yanga na Azam, lakini msimu huu umeonekana ni wa mabadiliko.

Mbali na kuwa bado timu hizo zina wachezaji wakongwe, lakini vijana wameleta chachu kubwa, kwani si wale ambao wanaingia kipindi cha pili kwa sababu tu mchezaji fulani kachoka, ila wameonekana kuleta vitu tofauti na kuanza kuwa tegemeo, hawa ni wachache kati ya wengi walionyesha ubora na kutoa changamoto kubwa...

**#1. Aboutwalib Mshery - Yanga**

Ni golikipa wa Yanga ambaye amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Mtibwa Sugar. Ni kinda wa miaka 21 tu. Ni mmoja wa wachezaji vijana wanaofanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania mpaka sasa, akianzia na Mtibwa ambako amecheza nusu msimu kabla ya kuhamia Yanga.

Awali, mashabiki wa Yanga walikuwa na wasiwasi baada ya kipa namba moja Djigui Diarra kwenda kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) nchini Cameroon akiwa na kikosi cha timu ya Taifa ya Mali.

Haraka wakamtwaa Mshery kuja kuchukua nafasi yake, na hadi sasa hajawaangusha. Amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu, kile kile ambacho alikuwa nacho Mtibwa Sugar.

**#2. Tepsi Evans - Azam FC**

Ana umri wa miaka 19 tu, lakini tayari ameshaanza kujichukulia umaarufu kwenye soka la Tanzania akiwa bado kinda kabisa. Ni mmoja wa wachezaji zao la Azam FC, akijiunga na 'akademi' hiyo mwaka 2016, lakini msimu huu anacheza Ligi Kuu.

Kwa nusu msimu tu, amekuwa moja ya wachezaji waliotia fora na kuvutia mashabiki wengi, akiwa anacheza kama kiungo mshambuliaji na pia winga. Hivi majuzi ameongezwa mkataba wa mwaka mmoja na timu yake, sasa utamalizika 2025, badala ya 2024.

**#3. Peter Banda - Simba**

Amesajiliwa msimu huu kutoka FC Shariff ya Moldovia, ambako alikuwa akicheza kwa mkopo, akitokea Nig Bullets ya Malawi.

Ingawa bado hajaonekana kupata nafasi sana kwenye kikosi cha Simba, lakini zile dakika chache anazoingia anaonekana ni mchezaji mwenye kipaji na hatari, ambaye anaweza kuibeba timu hiyo siku za usoni.

Ni suala la muda tu, pia anaweza kuipatia kipato klabu kwa kumuuza kwa klabu kubwa, kutokana na umri wake wa miaka 21 tu alionao. Banda, raia wa Malawi pia anaichezea timu ya taifa ya nchi yake na alicheza baadhi ya mechi kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) ambazo zilihitimishwa jana kwa Misri na Ivory Coast kucheza fainali jana.

**#4. Denis Mkane - Yanga**

Kinda huyu mwenye miaka 19, alisajiliwa na Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili msimu huu. Ni mmoja wa winga machachari ambaye hakukaa sana kwenye klabu yake ya Biashara United.

Achana na mechi ya kwanza dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, lakini alifanya makubwa kwenye michuano ya awali ya Kombe la Shirikisho, akifunga bao moja kwenye moja ya mechi ya timu hiyo iliyochezwa, kabla ya kujitoa yenyewe kwa kutokwenda kucheza mechi dhidi ya Al Ahly Tripoli ugenini. Akiwa Biashara United amefanya makubwa ikiwa ni pamoja na kupachika mabao.

Yanga imemsajili na kuonyesha uwezo mkubwa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, kabla ya kuwa majeruhi kwa sasa.

Hajacheza mechi yoyote ya ligi akiwa Yanga, lakini wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wana matarajio makubwa naye kutokana na umri wake, wakimfananisha na winga wa zamani wa timu hiyo, Mrisho Ngassa.

**#5. Pachal Msindo - Azam**

Huyu ni beki wa kushoto wa Azam FC ambaye naye amekuwa mmoja wa wachezaji wa kutegemewa msimu huu.

Pia naye amepandishwa kutoka chini kwenye 'akademi' ya alipojiunga mwaka 2016 kama Tepsi. Ni mmoja wa wachezaji ambao wanaonekana kuwa hazina kubwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars baadaye kama kiwango chake kitaendelea kuwa hivi. Ana miaka 18 tu.

**#6. Israel Patrick - Simba**

Anaichezea Simba na Timu ya Taifa, Taifa Stars. Ana umri wa miaka 21 sasa, na anaonekana ameanza kuaminika taratibu kwenye kikosi cha mabingwa hao.

Mwenda, ambaye ameshawahi kuzichezea klabu za Alliance, lakini Simba ikimsajili mwanzoni mwa msimu huu akitokea KMC.

Ana uwezo wa kucheza beki zote za pembeni, lakini wasichokijua wengi ni kwamba ana uwezo mkubwa wa kupiga vizuri penalti, na faulo, kiasi kwamba ameshawahi kuifungia Alliance mabao mengi, pamoja na bao moja Stars. Anaonekana anaweza kuwa mrithi sahihi wa Shomari Kapombe.

**JE, WAJUA?**



NYOTA wa zamani wa Cameroon, Samuel Eto'o bado ndiye anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao mengi (18) kwenye michuano ya AFCON yakitokana na mechi 29, akifuatiwa na Laurent Pokou (mabao 14, mechi 14), Rashidi Yekini (mabao 13, mechi 24), Hassan El-Shazly (mabao 12, mechi 10) na Didier Drogba (mabao 11, mechi 24).



HABARI DODOMA

# Watupa taka ovyo watangaziwa kiama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imewaonya wananchi wenye tabia ya kutupa taka ovyo ikiwamo pampasi kuwa haitasita kuwakamata na kuwachukulia hatua kwa kuchafua mazingira.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, alitoa onyo hilo jana zoezi la usafi na upandaji miti lililofanyika Kata ya Chang'ombe kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya usafi na upandaji miti Dodoma.

"Nisisitize wanaotupa pampasi mpo hapa hapa, mnaotupa taka mpo hapa hapa nawatumia salamu nitawakamata nina askari wa kutosha nimeajiri wiki iliyopita askari 80 na Jumatatu (leo) ninaleta askari 40 kwa ajili ya Chang'ombe tu kwa hiyo ndugu yangu unayetupa pampasi ninaruka na wewe," alisema.

Aliwataka wananchi kuzingatia usafi na kukumbushana wajibu wa kutunza mazingira.

"Pia hawa askari ambao wanavaa kiraia watakuwa na pingu watashughulika na wale wenye mifugo ambao wanatembeza katikati ya Jiji na kuua miti iliyopandwa, mtafute maeneo tumetenga maeneo ya kufugia yapo," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki shughuli za usafi.

"Tujitokeze kwa wiki kila siku ya usafi nimezunguka kata nyingi hapa nimeona mmejitokeza kwa wingi, mwendelee hivi, msiwe mnajitokeza tu kwa ajili ya kuonekana kwenye TV usafi uwe sehemu ya maisha yetu siku zote," alisema.

Naye Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Dk. Franklin Rwezimula, alisema usafi umekuwa ukifanyika kila Jumamosi.

"NEMC tumekuwa tukishiriki kwenye mazoezi yote ya usafi, licha ya kusimamia shughuli nzima ya mazingira tunakuwa mfano kwa kushiriki kushirikiana na viongozi wa Mkoa, tunashirikiana vizuri sana na Jiji la Dodoma, kwa sasa tupo kwenye programu ya kuikijanisha Dodoma tutakuwa na wiki nzima ya kupanda miti na kufanya usafi ili Dodoma iwe ya kijani," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mazingira wa Jiji la Dodoma, Ally Mfinanga, alisema wameendelea kutekeleza maagizo ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyoyatoa ya kuhakikisha mazingira ya Jiji yanakuwa safi.

"Aliagiza suala la usafi na upandaji wa miti kama mnavyojua Dodoma tuna programu ya Dodoma ya kijani na huu ni msimu wa mvua ni miongoni mwa shughuli kubwa zinazofanyika kipindi hiki, tumekutana leo kwenye Zahanati ya Chang'ombe ili kupeana hamasa kufanya usafi na tunakuwa na viongozi, tunashirikiana kwa karibu na NEMC," alisema.

Aidha, alisema baada ya usafi wananchi hupewa fursa ya kutoa kero zao na kusikilizwa.

# Sera mpya ya Taifa ya mazingira yaandaliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeandaa Sera mpya ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 baada ya kukamilisha mapitio ya mwaka 1997.

Sera hiyo inatarajiwa kuzinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango Februari 12, mwaka huu, jijini Dodoma.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mary Maganga, alisema

sera hiyo imejumuisha masuala ya mazingira yaliyokuwamo katika sera ya mwaka 1997 na masuala mengine mapya.

Alitaja masuala hayo ni udhibiti wa taka za kielektroniki, usimamizi na matumizi ya kemikali, udhibiti wa uchafuzi katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, mabadiliko ya tabianchi,

usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa na

udhibiti wa viumbe vamizi.

"Hivyo, Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 imeongeza wigo wa masuala na changamoto za mazingira zinazopaswa kufanyiwa kazi katika kipindi husika ili kuleta maendeleo endelevu. Vilevile, sera mpya imezingatia changamoto mpya za kimazingira zinazoendelea kujitokeza kutokana na mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi, kijamii na kimazingira yanayoendelea duniani," alisema.

Hata hivyo, alisema kutakuwa na

wiki ya uzinduzi wa sera hiyo itakayoanza tarehe Februari 7 hadi 12, mwaka huu ambapo shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira zitafanyika ikiwa ni sehemu ya masuala ya msingi yanayoelekezwa katika sera mpya.

Alisema lengo ni

kurejesha hali ya asili ya mazingira iliyoharibika kutokana na shughuli za kibinadamu kwa kupanda miti.

"Ili kuwa na mazingira safi kutakuwa na shughuli za usafi wa mazingira zinazolenga kuboresha afya ya jamii na elimu ya utenganishaji taka kwa ajili ya udhibiti wa taka ngumu na kuwezesha urejelezaji wa taka kwenye bidhaa na huduma mbalimbali," alisema.

Alisema kutafanyika upandaji miti jijini Dodoma, kufanya usafi pembezoni mwa barabara mbalimbali, kutoa elimu kuhusu utenganishaji wa taka na kufanya usafi katika soko la Chang'ombe na utoaji wa elimu ya mazingira kwa wananchi na wadau kupita vyombo vya habari.



Mratibu wa mradi wa kuhamasisha utolewaji wa huduma shirikishi za afya kwa watu wenye ulemavu jijini Dodoma, Askofu Frank Sarungi wa Kanisa la Bethel Baptist Deaf Church of Tanzania, akizungumza kwa kutumia lugha ya alama na madaktari wa vituo vya afya jijini humo (hawapo pichani), jinsi ya kuwasiliana na wenye tatizo la uziwi kwenye mafunzo yaliyofanyika jana. Katikati ni Mganga Mkuu wa Mkoa Hospitali ya Dodoma, Dk. Mbelle James na Dk. Irere Joseph wa hospitali hiyo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jiji latakiwa kutenga maeneo vitega uchumi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetakiwa kutenga maeneo ya vitega uchumi kwa ajili ya vikundi mbalimbali vya ujasiriamali wanaokopeshwa mikopo ya asilimia 10 ili kupata masoko ya bidhaa wanazozizalisha.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimwer, alitoa maelekezo hayo juzi alipokuwa akikabidhi hundi ya ya mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 817.4 iliyotolewa na Jiji hilo kwa ajili ya vikundi 78 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Shekimweri alisema pamoja na juhudi kubwa inayofanywa na Jiji za kuvikopesha vikundi hivyo ni muhimu kutengewa maeneo ili kupata masoko yanayozalishwa na kuuza bidhaa zao.

"Ni wakati sasa kwenu nyinyi halmashauri ya Jiji kutenga maeneo ya kibiashara ikiwamo viwanda kwa ajili ya vikundi hivi mnavyovikopesha kwa asilimia kumi, ili bidhaa wanazotengeneza waweze kupata masoko na kukuza mitaji yao, na hii itawawezesha pia kurudisha mikopo yao kwa wakati," alisema.

Alivitaka vikundi hivyo kutumia mikopo hiyo kwa malengo yaliyokusudiwa na kurejesha kwa wakati ili kujiepusha kufilisiwa mali zao walizodhamini.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana wa Jiji hilo, Asha Shame Vuai, alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 Sh. milioni 817.4 zimetolewa na Jiji kwa ajili ya kukopesha vikundi hivyo ambapo kati ya fedha hizo Sh. milioni 395 zimekopeshwa kwa vikundi 46 vya wanawake.

Pia alisema kwa upande wa vikundi vya vijana Sh. milioni 364 zimetolewa huku watu wenye ulemavu wakipata Sh. milioni 58.4.

Aliwataka wanaokopa kukumbuka kurejesha kwa wakati, badala ya kubweteka na kujiona umaskini umeondoka.

"Uzuri wa kukopa ni kurudisha kwa hiari badala ya kusubiri kunyang'anywa mali zenu na kuleta usumbufu usio kuwa na tija kwenye mikopo," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, aliwataka kujenga uaminifu wa kuzitumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ambayo ni sahihi ili wawe mabalozi kwa wale wanaohitaji kukopa.

Alisema malengo ya mikopo inayotolewa na halmashauri ni kujiimarisha kiuchumi, hivyo fedha hizo zinatakiwa kutumika kwa uangalifu na si kufanya anasa.





# Mbeya ilivyopunguza idadi ya vifo vya uzazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umefanikiwa kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na matatizo ya uzazi kutoka 133 kati ya vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2015 na kufikia vifo 102 kwa mwaka 2021.

Pia imepunguza idadi ya vifo vya watoto wachanga kutoka 14 hadi kufikia nane.

Aidha, idadi ya wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya huduma za afya imeongezeka kutoka asilimia 77 ya mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 85 kwa mwaka 2021 na kufanya idadi ya wajawazito 70,404 kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma kati ya wajawazito 83,058 waliolengwa.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Benson Sanga ambaye ni Ofisa Lishe wa Mkoa juzi akizungumza na Nipashe, alisema idadi hiyo inatokana na jitihada za serikali katika kujenga vituo vya huduma za afya, hospitali na zahanati.

Alisema miongoni mwa mafanikio katika sekta ya afya ni pamoja na ongezeko la vituo vya afya vinavyotoa huduma za dharura kwa wajawazito kutoka vituo viwili kwa mwaka 2015 hadi vituo 11 kwa mwaka 2021.

Katika utawala wa Rais wetu mpendwa wa Tanzania Samia Suluhu Hassan, mkoa umefanikiwa kuongeza hospitali zenye vyumba vya kutolea huduma za watoto wachanga wagonjwa (NCU) kutoka kimoja hadi kufikia tisa vilevile vifo vya watoto wachanga chini ya miaka mitano kutoka vifo saba katika kila vizazi hao 1,000 (2015) hadi kufikia vitano kwa mwaka (2021).

Aidha, Sanga alisema licha ya serikali kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga miundombinu rafiki vilevile imefanikiwa upatikanaji wa dawa muhimu 30 katika Mkoa wa Mbeya ambapo awali ulikuwa asilimia 93.2 na kwamba hadi kufikia Oktoba hadi Desemba mwaka 2021 hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma ulikuwa asilimia 94.6.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya, imetoa kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya Septemba 2021.

Hivi karibuni Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, kupitia kikao cha kamati ya ushauri ya Mkoa aliomba serikali kuajiri watumishi katika vituo vya afya na zahanati kwa maelezo kuwa kuna upungufu mkubwa.

Alisema serikali imejitahidi kujenga miundombinu rafiki ya kutolea huduma, lakini kikwazo ni kukosekana na kwa wataalamu wa afya kwa madai kuwa maeneo mengi kuna mhudumu mmoja tu hali inayopunguza ufanisi katika kuwahudumia wagonjwa.



Ofisa Maendeleo ya Jamii, Mkoa wa Mbeya, Stella Kategile (kushoto), akikata keki wakati wa kufunga kikao kilichowahusisha wanahabari vijana, wahariri na watumishi wa asasi mbalimbali za kiraia mwishoni mwa wiki katika ukumbi wa GR hoteli jijini Mbeya (wapili kushoto), Zamda Mafimba wa Shirika la We World. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Tani 3,918,876 mazao ya chakula kuzalishwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umelenga kulima jumla ya hekta 557,183 za mazao ya chakula yanayotarajiwa kuzalisha tani 3,918,876 huku mazao ya biashara ikikadiriwa kulimwa hekta 57,098 na kuzalisha tani 62,124 katika mwaka 2021/2022.

Ofisa Kilimo Mkoa wa Mbeya, Marianus Ngui, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki na kufafanua kuwa taarifa za awali kutoka kwenye halmashauri zinaonyesha kuwa huenda malengo yasikifiwe kama ilivyotarajiwa kutokana na uhaba na mtawanyiko wa mvua usioridhisha kwenye maeneo mengi ya mkoa pamoja na kupanda kwa gharama za pembejeo za kilimo.

Akifafanua malengo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara katika kila halmashauri, alisema Busokelo wamelenga kulima hekta 42,711 na kuvuna tani 292,317 ya mazao ya chakula pamoja na kulima hekta 4,962 ya mazao ya biashara na kuvuna tani 13,964.

Chunya imepanga kulima hekta 102,741 na kuvuna tani 348,911 ya mazao ya chakula huku hekta 20,421 ya mazao ya biashara ikipangwa kulima na kuvuna tani 11,301.

Mbarali imepanga kulima hekta 136,341 na kuvuna tani 603,936 ya mazao ya chakula na kulima hekta 1,681 ya mazao ya biashara na kuvuna tani 8,570.

"Kwa kuzingatia kigezo cha usalama wa chakula na lishe Mkoa wa Mbeya, ulizalisha asilimia 94 ya malengo ya mazao ya chakula kwa mujibu wa matokeo ya idadi ya watu mwaka 2021," alisema Ngui.

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa chakula kimkoa, alisema ni tengefu na endelevu na kwamba akuna tishio la upungufu wa chakula hivyo wananchi wanasisitizwa kuendelea kutumia vyakula kwa uangalifu ili kujihakikishia usalama na uhakika wa chakula muda wote.

Aidha, katika taarifa yake Ngui alishauri kuwa kwa maeneo ambayo bado kuna upatikanaji hafifu wa mvua katika msimu wa kilimo 2021/2022 kustawisha mazao jamii ya mizizi hususani mihogo ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula.

Kuendelea kutunza vizuri hifadhi ya mazao ya chakula yaliyoko ngazi ya kaya na kuepuka kuuza mazao ya chakula bila sababu za msingi pamoja na wakulima kutumia akiba ya fedha walizozipata kutokana na uuzaji wa mazao ya biashara kununua chakula cha kutosheleza mahitaji katika familia zao.

# Wamfagilia RC kuwaondolea kero ya tozo kutembelea fukwe Z/Nyasa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WAWEKEZAJI wa hoteli katika mwambao wa Ziwa Nyasa wilayani Kyela, wamemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kuondoa tozo za ushuru wa mageti kwa wananchi wanaotembea fukwe zilizoko Ziwa Nyasa.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Meneja wa Hoteli ya Landmark, Amos Lugano, alisema uamuzi wa Homera kuondoa tozo za ushuru ndani ya fukwe za Ziwa Nyasa kumechangia idadi kubwa ya watalii kutembelea maeneo hayo.

Alisema uamuzi huo ni ishara kwamba sasa sekta ya utalii kupitia fukwe za Ziwa Nyasa wilayani Kyela inazidi kukua siku hadi siku na kuongeza idadi ya watalii kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea.

Alisema kitendo cha serikali kuondoa tozo hizo, kimekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha sekta ya utalii na uhusiano mzuri kwa wawekezaji ambao sasa katika fukwe za Matema unazidi kukua siku hadi siku.

"Hakika tunajivunia kuwa na Mkuu wa Mkoa Juma Homera amekuwa rafiki kwetu sisi wawekezaji mbali na kuondoa tozo kwa wananchi wanaotembelea fukwe hizi, lakini pia amekuwa akitutafutia wateja kutoka maeneo mbalimbali," alisema Lugano.

Aliongeza kuwa awali kabla ya serikali kuondoa ushuru kwenye geti la kuingilia katika fukwe za mwambao mwa Ziwa Nyasa upande wa matema ilikuwa lazima walipie kila mmoja shilingi 1,000, lakini sasa baada ya kuondoa tunapokea watalii wengi.

Akizungumzia upatikanaji wa nishati ya umeme, Meneja huyo alisema kwa wameunganishwa na huduma hiyo baada ya serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kuwasogezea huduma hiyo na kuwasaidia kuondokana na adha ya kutumia genereta ambapo walikuwa wanatumia kiasi cha shilingi milioni mbili kwa mwezi kununua mafuta.

Miongoni mwa wadau wanaotembelea fukwe hizo, Beatrice Mwampaja, ambaye ni mkazi wa Ipinda aliwahamasisha wengine kutembelea maeneo hayo ili kujionea mandhari mazuri ambayo kwa namna moja au nyingine husaidia kupunguza msongo wa mawazo.





## SMZ yaapa kupambana na saratani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazurui, amesema serikali itachukua hatua kuhakikisha inapambana na ugonjwa wa saratani.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani yaliofanyika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Mjini Zanzibar, alisema ugonjwa wa saratani bado upo Zanzibar ambao unawaathiri wananchi wote kwa kasi kubwa kutokana na mazingira yaliyowazunguka.

Alisema kuenea kwa ugonjwa huo kunachangiwa na hali ya hewa, vyakula, matumizi ya tumbaku, pombe na kutofanya mazoezi.

Mazurui alsema kuwa saratani ya matiti na shingo ya kizazi ndizo zinazoongoza kwa wanawake na saratani ya tezi dume kwa wanaume Zanzibar.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2017 wagonjwa wa saratani ya matiti walikuwa 62 na mwaka 2021 uchunguzi umegundua wagonjwa 62 wa maradhi hayo, huku 57 kwa mwaka 2017 na mwaka 2021 ni 37 wakati kwa tezi dume ni 36 kwa mwaka 2017 na kwa mwaka 2022 ni 30.

Aidha, alisema hatua mbalimbali zinachukuliwa kupunguza idadi ya wagonjwa wa saratani ikiwamo utoaji wa elimu wa kujikinga na saratani, kuongeza vifaa tiba katika kitengo cha saratani, uongeza idadi ya madaktari pamoja na kuondoa changamoto ya upatikanaji wa dawa za ugonjwa huo.

Alisema ugonjwa wa saratani matibabu yake yana gharama kubwa, hivyo wananchi hasa wanyonge wanahangaika katika kutafuta tiba ndani na nje ya nchi, hivyo serikali itawawekea mazingira mazuri katika kuwasaidia ili kupunguza gharama.

Mfamasi Abdulrahmani Mashauri kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, aliiomba wizara kutoa kliniki maalum ya huduma ya uponyaji (palliative care), kuendeleza huduma za saikolojia tiba na saikolojia imani, kufufua na kuendeleza uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na matiti pamoja na mkakati endelevu wa upatikaji wa dawa za saratani.

Alisema wagonjwa wa saratani waliopata huduma katika kliniki ya saratani pekee katika kipindi cha miaka minne ni 1,492, wakiongoza wagonjwa wa saratani ya matiti ambao ni 274, shingo ya kizazi 262, tezi dume 215 na mfumo wa chakula 160 ambapo saratani ya damu ni 126.

Hata hivyo amesema hivi sasa katika kupambana na ugonjwa huo changamoto kubwa ni kutotekelezwa kwa ufanisi mpango mkakati wa saratani wa mwaka 2018/2023), kusuasua mradi wa huduma za mionzi tiba, kukatika muungano wa huduma za saratani ngazi ya wizara pamoja na uhaba wa wafanyakazi katika kitengo cha saratani.

# Waziri ataja dawa ya makosa ya barabarani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, amesema Zanzibar inahitaji kuwa na adhabu ya papo kwa papo ili kupunguza makosa ya uvunjifu wa sheria ya barabarani ambayo yanasababisha ajali.

Akizungumza katika kikao kazi kati ya Jeshi la Polisi na wadau wa vyombo vya usafiri baharini na nchi kavu uliofanyika Mjini Zanzibar, alisema suala hilo tayari limeshajadiliwa na limefikia katika hatua nzuri na wizara yake kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani itatumia mfumo unaotumika Tanzania Bara katika utekelezaji wa adhabu hizo.

Waziri huyo alizitaka mahakama zihakikishe zinatekeleza sheria kikamilifu ili kukomesha uvunjifu wa usalama barabarani na madereva hawaogopi kupelekwa mahakamani kwa sababu hata wakifikishwa hawachukuliwi hatua badala yake huachiwa.

Pia alilitaka Jeshi la Polisi kuondoa aibu kwa madereva wanaopatikana na makosa kuachiwa bila ya kuchukuliwa hatua stahiki. "Aidha, niwaombe Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kuwachukulia hatua kwa kuwafutia leseni madereva watakaoonyesha kutojali sheria za usalama barabarani, ikiwa ni adhabu kwao na wengineo wapate funzo na kuepukana na tatizo hili," alisema.

Kuhusu alama za barabarani, waziri huyo alisema wizara yake imeshakusanya taarifa za mahitaji ya alama hizo Unguja na Pemba na kwa hatua ya kwanza wanategemea kuweka alama katika kila maeneo hatarishi kwa usalama wa barabarani na baadaye kueneza alama hizo kwa maeneo yote yanayohitaji kuwekewa.

Naye Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, Wilbrod Mutafungwa, alisema Jeshi la Polisi kazi kubwa ni kusimamia sheria ili barabara iwe salama, vifo visitokee na hata kama ajali itatokea majeraha yasiwe makubwa.

Alisema ili askari wa kikosi hicho wafanye kazi vizuri, lazima alama za barabarani ziwapo kwa sababu ndio mawasiliano pekee kati ya dereva na barabara.

"Taasisi husika lazima kuhakikisha alama za barabarani zinakuwapo kila mara ili kumfanya dereva kuwa na utii wa sheria, kanuni na taratibu za usalama wa barabarani na kupunguza ajali," alisema.

Alisema ambao wanavunja sheria za barabarani wasionewe aibu na wachukuliwe hatua ili kuendelea kusimamia maadili ndani ya Jeshi la Polisi hasa kwa askari wa usalama wa barabarani ili kuwajengea uwezo wa utoaji wa huduma bora na kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

Aidha, aliwapongeza madereva wanawake kutokana na umakini wa utii wa sheria barabarani ikilinganishwa na madereva wanaume.

Hassan Mchangama, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), alisema haki za abiria zipo kwa mujibu wa sheria, hivyo kuhakikisha watoa huduma wa usafiri wa baharini na nchi kavu wanatekeleza haki za abiria ili kupata haki zao na kufika wakiwa salama.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa (katikati), akikata keki iliyoandaliwa na wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kampasi ya Karume, baada ya kuzungumza nao katika warsha ya klabu ya jinsia na maendeleo chuoni hapo, Bububu Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## TAMWA yatoa msimamo watoto wa kike wanaobakwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amesema hakubaliani na mawazo ya baadhi ya watu wanaotaka mtoto wa kike kuanzia miaka 15 aliyedhalilishwa kwa kubakwa na yeye afungwe jela badala ya kufungwa mwanaume pekee.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika warsha ya klabu ya jinsia na maendeleo ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kampasi ya Karume Zanzibar huko Bububu nje ya Mji wa Zanzibar.

Alisema kuwa baadhi ya watu wamekuwa na maoni hayo wakidai kuwa sheria ya mtoto ibadilishwe ili mtoto wa kike kuanzia miaka 15 wafungwe endapo watajihusisha na masuala ya kimapenzi jambo ambalo yeye halafiki.

"Mkamatwa na ngozi ndio mwizi, kwa hiyo watoto wa kike wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji wasifungwe, waendelee kufungwa hao washtakiwa ili kukomesha vitendo hivyo," alisema Dk. Mzuri.

Alisema kuwa endapo unazungumzia mtoto wa kike afungwe utamlinda vipi mwanamke na mtoto wa kike kwa sababu watoto wa kike wanaojihusisha na mapenzi huwa ni waathirika tokea wakiwa na umri mdogo kwa kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Alisema lazima kuwe na mbinu nzuri za kuwalinda watoto ambao kwa bahati mbaya wameshafanyiwa vitendo vya udhalilishaji, kuliko kutaka watoto wa kike nao wafungwe.

Aliwataka wanafunzi wa chuo hicho kuwa na malengo ya baadaye na kutojihusisha na vitendo viovu ambavyo vitasababisha kutofikia malengo yao.

Akisoma risala ya klabu ya jinsia na maendeleo ya chuo hicho, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Ali Hafidhh Iddi, alisema warsha hiyo imeandaliwa ili kukutanisha wadau wa masuala ya kijinsia na kujadili masuala yanayohusu jinsia katika jamii na kupata suluhisho kuhusu changamoto zinazoikumba jamii hasa wanawake na watoto.

Alisema jamii inahitaji mchango wa taasisi na wadau wa masuala ya jinsia ili kupambana na vitendo viovu na vya kikatili vinavyotendeka katika jamii.

"Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimeendesha tafiti zinazohusu masuala ya kijamii na kugundua suala la unyanyasaji wa kijinsia limeongezeka kwa kiasi kikubwa hasa kwa upande wa watoto na wanawake," alisema.

Mkuu wa kitendo cha klabu ya jinsia na maendeleo ya chuo hicho, Dk. Venance Kalumanga, alisema chuo kinatarajia kuwa na klabu za jinsia hadi katika shule za msingi na sekondari.

Alisema wimbi la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ni kubwa, hivyo halitaweza kuondolewa na serikali pekee bali na jamii nzima.

Alisema wanaofanyiwa vitendo vya unyanyasaji na ukatili wengi wao ni wale ambao wapo katika hali duni ya kimaisha na wenye umri mdogo hivyo ni vyema kushirikiana pamoja katika kutokomeza vitendo hivyo ambavyo ni kinyume na haki za binadamu.

Mkuu wa dawati la jinsia, Wilaya ya Mjini Magharibi Unguja, Mkaguzi wa Polisi Muhammed Mwadini Kificho, alisema bado elimu inahitajika kwa jamii kuhusu vitendo vya udhalilishaji.

Alisema kwa Januari pekee mwaka jana vitendo vya udhalilishaji 52 viliripotiwa katika dawati hilo na Januari kwa mwaka huu matukio 21 yameripotiwa na kwamba changamoto kubwa matukio mengi ya watoto wa kike huingiliwa kinyume cha maumbile.

## Shule Kilwa zapewa vifaa vya mil. 25/-

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE tano za Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi zimekabidhiwa vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 25 kwa ajili ya ujenzi.

Shule zilizokabidhiwa vifaa hivyo vilivyotolewa na Benki ya NMB ni shule za msingi za Somanga, Kiswere na Pungutini pamoja na shule za sekondari za Kilwa na Kiranjeranje.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kilwa ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, Meneja wa NMB Kanda ya Kusini - Janeth Shango, alisema wametoa vifaa hivyo ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa benki hiyo katika uwajibikaji kwa jamii.

Alisema maamuzi hayo ni katika kushirikiana na serikali katika kukabili vikwazo kwa sekta ya elimu kutokana na ukweli kwamba elimu ndio ufunguo mkuu wa maendeleo kwa taifa lolote duniani.

"Tunatambua juhudi za serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan za kusimamia upatikanaji wa elimu bora kwa nguvu zote huku akijikita katika kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma hizi mjini na vijijini, sisi kama wadau tunao wajibu wa kuunga mkono juhudi hizi," alisema Shango.

Alisema Benki ya NMB imekabidhi mabati 350, madawati 50, viti 100 na meza 100.

Alisema kwamba Shule ya Msingi Somanga imepatiwa mabati 200, Shule ya Msingi Kiswere imepatiwa mabati 150 na Shule ya Msingi Pungutini imekabidhiwa madawati 50. Aidha alisema Shule ya Sekondari Kilwa ilipatiwa viti 50 na meza 50 na Shule ya Sekondari Kiranjeranje viti 50 na meza 50.

"Sisi tunao wajibu wa kuhakikisha jamii inayotuzunguka inafaidika kutokana na faida tunayoipata," alisema Shango.

Kwa miaka kadhaa sasa, NMB imekuwa ikisaidia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi kwa kujikita zaidi kwenye miradi ya elimu (madawati na vifaa vya kuezeka), afya (vitanda, magodoro yake na vifaa vingine vya kusaidia matibabu) na kusaidia majanga yanayoipata nchi.

"Tunatambua kuwa ni kupitia jamii ndipo wateja wetu wengi wanapotoka, kwa hiyo kurudisha sehemu ya faida kwa jamii ni utamaduni wetu," alisema.

Kwa mujibu wa Shango kwa zaidi ya miaka saba sasa mfululizo NMB imekuwa ikitenga asilimia 1 ya faida yake kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii inayowazunguka.

Akipokea misaada hiyo, Ndemanga alisema kwamba msaada huo umekuja wakati mwafaka.

Aliishukuru benki kwa kujali wateja wake na kuwataka wazazi pia kujali watoto wao kwa kutumia Benki ya NMB kuweka amana zao ambapo faida hurejeshwa kwao wenyewe.

# ILO yabainisha wanawake vijana walivyoathirika zaidi UVIKO -19

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Kazi Duniani (ILO), limelalamikia janga la UVIKO - 19, limewaathiri kwa kiasi kikubwa wanawake vijana katika soko la ajira, ambao takwimu zake zinaonyesha ndio sehemu kubwa ya waliojiajiri duniani.

Ripoti iliyotolewa mapema mwaka huu na ILO, kuhusu Ajira Duniani na Mtazamo wa Kijamii 2022, imebainisha hayo na kwamba kwa kipindi cha mwaka jana, wanawake hao waliathiriwa kutokana na uchumi kudhoofika karibu kila nchi, bila kujali hali ya maendeleo.

Mkurugenzi Mkuu wa ILO, Guy Ryder, kwenye muhtasari wake katika ripoti hiyo, alisema taarifa hiyo inatoa tathmini ya kina na jinsi ya kufufua soko la ajira duniani, ikiakisi mbinu tofauti za kitaifa kukabiliana na janga la UVIKO - 19.

"Ripoti inachanganua mifumo ya kimataifa, tofauti za kikanda na matokeo katika sekta zote za kiuchumi na vikundi vya wafanyakazi. Ripoti hii pia inatoa makadirio ya soko la ajira kwa mwaka 2022 na 2023.

"Janga la UVIKO - 29, ni changamoto zaidi katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030), ni muhimu serikali na mashirika ya waajiri na wafanyakazi, wawe pamoja na dhamira mpya ya kukabiliana na changamoto hizi.

Ripoti hiyo, inabainisha kwamba katika nusu ya pili ya mwaka 2021, kasi ya soko la ajira duniani ilipungua ikisema hali hiyo inatokea huku janga la UVIKO-19, likiingia mwaka wa tatu.

Inabainisha kwamba, mwaka 2021 kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN-Women) na Shirika la Mpango wa Maendeleo Duniani (UNDP), ilikadiria takriban wanawake na wasichana milioni 435 duniani waliishi chini ya dola 1.90 kwa siku, huku milioni 47 wakirudi kwenye kundi la umaskini.

Ripoti inasema, sehemu kubwa ya wanawake katika nchi zinazoendelea uchumi wao hutegemea ajira inayohusishwa moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja na minyororo ya ugavi, ikibainisha kwamba wanawake ni zaidi ya asilimia 70 ya wafanyakazi wote duniani, walioko katika sekta ya afya na huduma za matunzo.

Pia inasema katika kipindi hiki cha janga, Juni mwaka jana nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, zilipitisha wito duniani kuchukua hatua na mapendekezo kisera ili kuleta ahueni kwa nchi zilizoathiriwa na UVIKO - 19.




Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, Shaibu Ndemanga, akipokea msaada wa vifaa vya kuezekea, madawati, viti na meza kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, vyenye thamani ya Sh. milioni 25 kwa ajili ya shule tano za msingi na sekondari wilayani humo. Kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Kilwa, Ally Mohamed Mng'umba na Meneja NMB Kilwa, Nelly Masisi.

# Trafiki wanaodai rushwa waonywa

**Na Mohab Dominick, SIMIYU**

KAMANDA wa Polisi mkoani Simiyu, Blasius Chatanda, amelitaka Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani katika mkoa wake kutojihusisha na vitendo vya kupokea rushwa kutoka kwa madereva wenye makosa mbalimbali wanaposimamia sheria za usalama barabarani.

Amewataka askari wote wa mkoa huo watosheke na mishahara wanayolipwa na serikali kwani kitendo cha kupokea rushwa ni ukiukwaji wa maadili ya kazi zao ikiwa ni kulinda viapo vyao walivyoapa wakati wakikabidhiwa majukumu hayo.

Kamanda Chatanda aliwaambia waandishi wa habari kuwa kwa askari yeyote katika mkoa wake kama atabainika kwenda kinyume cha maadili ya kazi yake, hatakuwa na salia mtume, bali atachukua hatua za haraka pamoja na kumfikisha mahakamani.

Chatanda alitoa onyo hilo juzi, alipokuwa akijibu maswali kwa waandishi wa habari juu ya tuhuma za rushwa barabarani kwa askari wake wa Usalama Barabarani kutoka Kituo cha Polisi Lamadi kilichoko Wilaya ya Busega juu ya malalamiko kutoka kwa madereva wa mabasi yaendayo Mwanza- hadi Musoma dhidi ya askari (jina tunalo) kwa kujihusisha na vitendo vya kuomba rushwa kwa madereva na kuwalipisha faini mara mbili.

"Ikionekana askari wangu anajihusisha na vitendo vya rushwa sitomwacha salama, nitamchukulia hatua za kinidhamu ikiwamo kumfikisha mahakamani ili taratibu zingine zifuate, lakini niwasihi madereva nao waachane na msemo wao penye uzia penyeza rupia kwani nao wamekuwa chanzo," alisema Kamanda Chatanda.

Kamanda Chatanda alisema kuwa wakumbuke kuwa kutoa na kupokea yote ni makosa kwa hilo askari wake hatavumiliwa iwapo atabainika kujihusisha na vitendo hivyo.

"Haiwezekani serikali ikulipe vizuri halafu baadaye ukachukue hela kwa mwananchi wa kawaida anayehangaika na kamchomoko ili familia yake ipate kuishi, lakini kwa upande mwingine madereva nao wasiozingatia sheria za usalama barabarani ni zaidi ya jambazi anayetumia silaha," alisema.

Awali madereva wa mabasi kutoka Mwanza, Lamadi hadi Musoma wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari kwa sharti la kutoandikwa majina yao gazetini, walimlalamikia askari huyo wa kituo cha Polisi Lamadi kuwatoza faini mara mbili jambo ambalo linawakera.

"Kwa kweli huyo afande amekuwa kero kubwa kwa madereva, hasa sisi tunaotoka Mwanza kupita hapa Lamadi tukielekea Musoma - Sirali kikubwa tunachoomba serikali isikie kilio chetu tukifika hapa Lamadi ni tatizo kwake anapenda virushwa vidogo vidogo ukamnyima unatengenezewa kosa utakalolipa faini kubwa hana maadili, mbona wengine hawatufanyii hivyo," alisema mmoja wa madereva.

HABARI KIMATAIFA

# Wakuu AU wajadili usalama wa chakula barani Afrika

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

KIKAO cha viongozi wa Umoja wa Afrika (AU), kimeanza mwishoni mwa wiki, mjini Addis Ababa, na kauli mbiu ya mwaka huu, ikisema "Kuimarisha Uwepo wa Lishe na Usalama wa Chakula katika Bara la Afrika.

Pia wamekutana ili kuimarisha mifumo ya uzalishaji chakula, mifumo ya afya na ustawi wa jamii kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya binadamu, kijamii na kiuchumi.

"Viongozi kutoka barani Afrika, walikusanyika kujadili masuala yanayoliathiri bara hilo, hasa janga la corona na ukosefu wa usalama.

Kikao cha 35 cha AU, kilianza Addis Ababa, ingawa kauli mbiu inaelezea kujenga uthabiti katika lishe na kujitegemea katika chakula, Covid-19 na usalama viko juu kwenye ajenda huku mapinduzi na ukosefu wa uthabiti wa kisiasa vikiendelea kuathiri wakazi kote barani Afrika.

Wakati akiwahutubia viongozi wa bara hilo, Musa Faki Mahamat, mwenyekiti wa AU, alisema Afrika ni miongoni mwa mabara yaliyopigwa vibaya na Covid-19.

Pia alielezea wasiwasi wake kuhusu ukosefu wa upatikanaji wa chanjo kwa Waafrika wengi.

Aliwaomba viongozi wa kiafrika kukisaidia kituo cha Afrika cha kudhibiti magonjwa.

Mwenyekiti Faki pia alieleza kuhusu kushuka kwa hali ya usalama barani Afrika, akisema AU inakabiliwa na kushindwa kitaasisi kwa sababu ya mapinduzi na uasi.

Aliomba taasisi za kikanda kufanya kazi kwa karibu sana na Umoja wa Afrika na mataifa wanachama wake kuachana na matumizi ya kisingizio cha mamlaka yao.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, pia ni miongoni mwa viongozi ambao walihutubia katika mkutano huo.

Katika matamshi yake, Abiy alisisitiza nia ya utawala wake kumaliza mzozo uliodumu kwa miezi 16 na waasi wa Tigray.

"Kama ishara ya nia njema, tumewaachilia washukiwa wa juu, huku tukiweka mazingira mazuri kwa mazungumzo. Sambamba na azimio letu la amani, hivi karibuni tulianzisha mjadala wa pamoja wa kitaifa kwa sheria rasmi.

"Nia yetu ya dhati kutafuta amani ya kudumu na katika nchi yetu bado litakuwa ndiyo kipaumbele chetu," alisema Abiy.

Abiy, aliwaomba viongozi kuunga mkono ombi lake kwa Afrika kuwa na uwakilishi wa kudumu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Kwa kuongezea, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres alihutubia katika kikao hicho kwa njia ya video.

Guterres alisema Afrika imeathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa wakati ikichangia chini ya asilimia tatu ya utoaji wa gesi chafu.

"Kuzungumzia ukweli wa janga hili, tunahitaji kukuza ufadhili na kukabiliana na hali hii barani humo. Ahadi ya Glasgow ya kuongeza ufadhili mara mbili kutoka dola bilioni 20 lazima utekelezwe," alisema Guterres.

Guterres alieleza anafanya kazi na jumuiya ya kimataifa kukidhi utashi wa mabadiliko ya hali ya hewa kwa Afrika.

Pia aliwataka viongozi wa Afrika kuwajumuisha vijana katika utawala wao na kuwaacha raia kutumia haki yao ya kisiasa na kidemokrasia.

Washiriki katika kikao cha 35 cha viongozi wa AU, wamemtaja kiongozi wa Senegal Macky Sall kama rais mpya wa AU.

**VOA**

## Ripoti: Walinda amani 24 wa UN waliuawa mwaka 2021

**New York,** MAREKANI

WANAJESHI 24 wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa pamoja na mfanyakazi mmoja raia wa umoja huo, waliuawa katika mashambulizi ya kuwalenga, mwaka jana.

Taarifa hiyo ni kwa mujibu wa ripoti ya shirika la wafanyakazi wa taasisi hiyo.

Miongoni mwa walinda amani waliouawa ripoti hiyo imeeleza wawili walikuwa ni wanawake.

Kwa mwaka wa nane mfululizo Mali imeongoza kwa vifo vya walinda amani, 19 wakiuawa mwaka jana.

Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), ilishika nafasi ya pili kwa vifo vya walinda amani wanne.

Mkuu wa shirika la wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa, Aitor Arauz alisema katika taarifa kuwa inasikitisha kuona kwa mara nyingine wafanyakazi wa UN na hasa wanajeshi wanaotumwa katika nchi zenye mizozo mikubwa wameendelea kuuawa.

Ofisa huyo alisema la kusikitisha zaidi ni kuwa hakuna aliyekamatwa wala kuwajibishwa kwa mauaji ya walinzi hao wa amani. **DW**

**Mkuu wa shirika la wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa, Aitor Arauz alisema katika taarifa kuwa inasikitisha kuona kwa mara nyingine wafanyakazi wa UN na hasa wanajeshi wanaotumwa katika nchi zenye mizozo mikubwa wameendelea kuuawa.**



Kijana akiimarisha paa la nyumba yake kwa kuweka matofali juu ya bati, kuepuka kuezuliwa na upepo mkali, mjini Antananarivo, nchini Madagascar, jana, kufuatia mamlaka za hali ya hewa nchini humo kutoa tahadhari ya kimbunga Bastirai. **PICHA: AP**

## Baraza la mpito la Guinea lafanya kikao cha kwanza

**Conakry,** GUINEA

BARAZA la mpito Guinea, ambalo lina jukumu la kuandaa kurejea kwa utawala wa kiraia baada ya mapinduzi ya kijeshi ya mwaka jana ya serikali ya Rais Alpha Conde, kilifanya kikao chake cha kwanza, mwishoni mwa wiki.

Shirika la habari la Ufaransa AFP limeripoti kuwa wanachama wote 81 wa baraza hilo la mpito la kitaifa, linalojulikana CNT, walihudhuria kikao hicho cha ufunguzi katika majengo ya bunge mjini Conakry.

Kikao hicho kilichofunguliwa na Rais wa CNT Dansa Kourouma na pia kuhudhuriwa na Waziri Mkuu wa mpito, Mohammed Beavogui, mtaalamu wa maendeleo, kilichukuwa saa kadhaa.

Katika hotuba yake, Kourouma alisema kuwa mabadiliko makubwa katika mifumo ambayo inawaleta wasomi madarakani na kuwaruhusu kusalia madarakani kwa muda usiojulikana ni tatizo ambalo lazima litatuliwe kwa uhakika.

Alitaka katiba itungwe katika hali ambayo haitarekebishwa kirahisi, akimaanisha Conde, ambaye alizua hasira kwa kubadilisha katiba ili kuwania muhula wa tatu.

**DW**

# MWANACHUO NIT KULIWAKILISHA TAIFA SHINDANO LA MISS UTALII DUNIA

**Na Dennis Fussi**

KAMATI ya Miss Utalii Tanzania imemtangaza mwanafunzi kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Angela Steven, kuliwakilisha taifa katika Mashindano ya Miss Utalii Dunia yatakayofanyika katika Jiji la Sarawak nchini Malaysia.

Angela ambaye kwa sasa anasoma shahada ya kwanza katika Usimamizi wa Usafirishaji na Usafiri (Logistics and Transport Management) kwenye chuo cha NIT ana umri wa miaka 24 na ana urefu wa sentimita 177.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Rais wa Miss Utalii Tanzania, Gideon Chipungahelo, alisema wana imani kubwa mlimbwende huyo ataliwakilisha vema taifa katika mashindano hayo makubwa duniani yatakayoanza katika Jiji la Sarawaki Novemba 13 hadi 27, mwaka huu.

"Angela anajiamini, na amedhamiria kufikia malengo yake. Kushinda katika walimbwende zaidi ya 150 ni matumaini ya Kamati yetu ya Miss Utalii Tanzania kuwa atakwenda na kurudi na taji la dunia," alisema Rais huyo.

Chipungahelo ambaye kamati yake iliandaa shindano la Dunia la Miss Utalii mwaka 2006 nchini, alisema: "Kamati yetu imeshaanda mipango mikubwa ya kumwezesha Angela kushinda taji hilo."

Chipungahelo alitabanaisha kuwa Miss Utalii Tanzania ni shindano lenye mafanikio zaidi nchini, kwani ni shindano la kwanza Tanzania kushinda taji la dunia.

> **"Vile vile Miss Utalii Tanzania, ni shindano pekee Tanzania ambalo limeshinda mataji ka tika kila shindano la dunia na kimataifa tuliloshiriki, na ni shindano pekee la urembo wa kitalii na kitamaduni Tanza nia," alisema rais huyo kwa kujiamini.**

"Angela alikuwa mshindi wa taji la Miss Utalii Tanzania 2021/2022, alilolishinda katika fainali za taifa zilizofanyika kwa njia ya mtandao Novemba 22, mwaka jana," aliongezea.

"Vilevile kupitia uwapo wa rais wa shindano hili katika bodi na uongozi wa mashindano mbalimbali ya dunia na kimataifa, warembo walioshinda nafasi zinazofuatia watatu nao watapata nafasi ya kuwakilisha Tanzania katika mashindano mengine ya dunia na kimataifa mwaka huu ili kutoa fursa ya kuitangaza zaidi Tanzania kimataifa," alimalizia.

Kwa upande wa Angela, aliwaambia waandishi wa habari kuwa anamshukuru Mungu kwa nafasi hii ya kipekee ya kuliwakilisha taifa. "Kwa maombi na sapoti ya Watanzania ninahakika nitaweza kuiinua juu bendera yetu na kuliwakilisha vema taifa letu la Tanzania."

Alisisitiza: "Ninafuraha sana kuiwakilisha Tanzania kwenye mashindano haya ya Miss Utalii Dunia kwa mwaka huu wa 2022, nikiamini kuwa nitaweza kushinda taji hilo na kuliletea sifa kubwa taifa letu la Tanzania.

"Matumaini yangu ni kwamba nitaondoka nchini nikiwa na malengo ya kufanya vizuri kwenye fainali hizo za dunia za Miss Utalii.

"Sitowaangusha Watanzania, waniombee dua siku ikifika ya mimi kuelekea kwenye mashindano hayo na mimi nawaahidi nitapambana kwa ajili ya kufanya vizuri," alisema Angela.

Angela ambaye alizaliwa mkoani Mara mwaka 1998, anasema kuwa alianza kujihusisha na sekta ya urembo akiwa bado binti mdogo kabisa huku akiwa na dhamira kuu katika mabadiliko chanya.

Aliongeza: "Pia ninatambua msaada mkubwa kutoka kwa uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji chini ya uongozi wa Mkuu wa Chuo, Profesa Zacharia Mganilwa."




Miss Utalii Tanzania, Angela Steven. **MPIGAPICHA WETU**

# *Hitimana aanika tatizo mabeki KMC*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa KMC, Thierry Hitimana, amesema mara nyingi mabeki wake hupoteza umakini wanapofanikiwa kupata bao, na ndiyo maana wapinzani wao hurudisha mabao mara tu wanapofunga.

Hitimana alisema hivyo baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya KMC dhidi ya Biashara United ikipigwa juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.

"Tukishafunga bao tunapoteza kabisa umakini na hata leo umeona baada ya kufunga sijui kama ilichukua hata dakika tano kabla ya wenzetu kurudisha. Lakini pamoja na hayo, kazi ya kujenga timu huwa haiji kwa siku moja, tutaendelea kukumbushana na mambo yatakaa sana, hata hivyo pamoja na hayo, leo sikuwa na baadhi ya wachezaji wangu tegemeo," alisema kocha huyo raia wa Rwanda.

Naye Vivier Bahati, Kocha Mkuu wa Biashara United, amesema mechi ilikuwa ngumu na anashukuru kwa sare aliyoipata kwa sababu alikuwa ugenini.

"Hata hivyo, tumepoteza nafasi nyingi za kufunga. Hatukuzitumia hasa kipindi cha kwanza na hii ndiyo imesababisha sare, hii imekwisha tunakwenda kujipanga na mechi inayofuata," alisema Mrundi huyo.

KMC ilianza kupata bao dakika ya 69, kupitia kwa straika wao tegemeo, Hassan Kabunda, lakini Biashara United ilisawazisha dakika tano baadaye kupitia kwa Collins Opare na kuifanya mechi hiyo kumalizika kwa sare.

Kwa matokeo hayo, KMC inakuwa kwenye nafasi ya 10 kwa pointi 16, huku Biashara United ikifikisha pointi 12, ikiwa nafasi ya 13, timu zote zikiwa zimecheza mechi 14.

# KMKM haishikiki kileleni Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MABAHARIA wa KMKM wamezidi kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar kwa kufikisha alama 36 baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KVZ katika mchezo wa kwanza wa mzunguko wa pili wa ligi hiyo yenye timu 16 uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Amaan.

Bao hilo la KMKM ni kama la zawadi kwao, kwani hawana budi kuelekeza shukran zao kwa beki wa KVZ, Ahmed Salum, ambaye alijifunga dakika 66 akiwa katika harakati za kuokoa.

Kwa matokeo hayo, KVZ sasa imeporomoka kutoka nafasi ya pili katika msimamo wa ligi mpaka ya nne ikisalia na alama zake 27 huku nafasi ya pili ikishikiliwa na timu ya Mafunzo iliyofikisha alama 30 baada ya juzi kuwafunga wenyeji Machomane katika Uwanja wa Gombani.

KMKM nayo imeendelea kushikilia rekodi ya kutofungwa katika michezo yake 16 iliyocheza tangu kuanza kwa ligi hiyo msimu huu ambayo imekuwa na ushindani hasa kwa klabu kutoka Unguja.

Akizungumza kwa furaha baada ya mechi hiyo, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, licha ya kupata alama tatu, alikiri kuwa mchezo huo ulikuwa mgumu katika dakika zote jambo ambalo lilisababisha kuwapo kwa rafu kutoka kwa wachezaji wa pande zote.

Kwa upande wa Kocha wa KVZ, Omar Kingi, alisema kupoteza mchezo huo kumeendelea kumpa nguvu ya kujipanga kwa michezo mingine na kuyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza.

Ligi hiyo itaendelea tena Jumatatu kwa kuzikutanisha timu ya Zimamoto dhidi ya Yosso Boys katika Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri wakati majira ya saa moja usiku Uhamiaji watarajiwa kupepetana na Taifa Jang'ombe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVER WAKOMAA NA CARVALHO
LIVERPOOL itafanya mazungumzo na Fulham mwezi huu kwa ajili ya mshambuliaji mwenye umri wa miaka 19, Fabio Carvalho, huku wakitaka kufikia makubaliano kabla ya msimu ujao. (***Football Insider***)

### MBADALA WA HAALAND
KAMA Barcelona itashindwa kumsajili Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, msimu huu wamemlenga Alexander Isak mwenye miaka 22 kutoka klabu ya Real Sociedad, Antony mwenye miaka 21 kutoka Ajax, pamoja na Lisandro Martinez mwenye miaka 24. (***Sport***)

### UNITED WAMFUATILIA RUDIGER
MANCHESTER United "wanafuatilia kwa karibu mambo yanavyokwenda" huku mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger akiripotiwa kukataa ofa ya hivi karibuni ya mkataba na klabu hiyo, ambapo atalipwa pauni 200,000 kwa wiki. (***Football 365***)

### LOGBO AWANIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL wanamfuatilia kwa karibu mchezaji wa klabu ya Le Havre mwenye umri wa miaka 17, Andy Elysee Logbo ambaye analinganishwa na mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku. (***Mirror***)

### GNABRY AGOMBEWA ULAYA
KLABU za Manchester United na Liverpool kwa pamoja zinamfuatilia kwa karibu winga wa Bayern Munich, Serge Gnabry huku kukiwa na mzozo wa mkataba baina ya klabu hiyo ya Ujerumani na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, wakati Barcelona na Real Madrid pia zikimtaka. (***Mirror***)

### ANTONIO ATAKA MSAIDIZI
MSHAMBULIAJI wa West Ham, Michail Antonio ameitaka klabu hiyo kuboresha kikosi chake kwenye safu ya ushambuliaji na kusajili mshambuliaji mwingine msimu huu. (***Teamtalk via The Footballer's Football Podcast***)

### MILAN, LIVERPOOL MBIO MOJA
AC Milan nayo ina matumaini ya kuwahi dau la Liverpool na kumsajili Fabio Carvalho huku klabu hiyo ya Italia ikiwasiliana na wawakilishi wake. (***Calciomercato***)

### WILSHERE ATOBOA SIRI ARSENAL
KIUNGO wa kati, Jack Wilshere mwenye umri wa miaka 30, ameeleza ni kwa nini ameendelea kuwa mchezaji huru kwa kufichua kuwa kocha wa Arsenal, Mikel Arteta "hamtaki" yeye asaini mkataba katika klabu hiyo. Wilshire amekuwa akifanya mazoezi na klabu yake hiyo ya zamani. (***Mirror***)

### ZLATAN KUSAINI MKATABA
MKURUGENZI wa AC Milan, Paolo Maldini, amesema mshambuliaji Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 40, atasaini mkataba mpya katika klabu hiyo. (***Goal***)

### WIJNALDUM ATAJWA ARSENAL
ARSENAL imetajwa kwamba inawania kumsajili mchezaji wa Paris Saint-Germain, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 31, baada ya nyota huyo kuachwa nje ya kikosi cha wachezaji 25 kwa ajili ya mechi yao ijayo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid. (***The Sun***)

### JONES ALITAKIWA WATFORD
KLABU ya Watford ilijaribu kumwinda mlinzi Phil Jones mwenye umri wa miaka 29 kutoka Manchester United, lakini hawakuweza kumpa kabla ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho la Januari. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GIROUD APAZA SAUTI MILAN IKIIFUMUA INTER

●●● Kama nilivyosema kabla ya mchezo, tulitarajia kupata bao moja au zaidi, unashinda mechi ya dabi...

**MILAN,** Italia

OLIVIER Giroud amebainisha kwamba, AC Milan "imerudi" baada ya kupata ushindi kwenye 'dabi' ya Jiji la Milan dhidi ya Inter Milan, juzi.

Giroud alifunga mara mbili na kupunguza gepu la pointi moja dhidi ya vinara wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Inter - ingawa 'Nerazzurri' hao wana mchezo mmoja mkononi wakati wakifungwa mabao 2-1.

Milan walitoka nyuma kwa bao 1-0 lililofungwa na Ivan Perisic na kupata ushindi huo muhimu.

Giroud raia wa Ufaransa alianza kwa kusawazisha dakika ya 75 na akafunga bao la pili na la ushindi zikiwa zimebakia dakika tatu mchezo kumalizika na kuwafanya vijana hao wa kocha, Simone Inzaghi kuondoka uwanjani kichwa chini.

Hata hivyo, Milan ilimpoteza nyota wake, Theo Hernandez aliyeonyeshwa kadi nyekundu katika dakika za mwisho za mchezo huo.

**"Kama nilivyosema kabla ya mchezo, hii ilikuwa mechi maalumu. Unashinda mchezo wa dabi, tulikuwa na wakati mgumu kipindi cha kwanza, lakini baada ya mapumziko kwa dakika 45, tulirudi mchezoni," alisema Giroud akiiambia DAZN.**

"Tulikuwa tunatarajia tungepata bao moja au zaidi, la kwanza lilikuwa la bahati, lakini la pili lilikuwa zuri sana kwa pasi safi ya (Davide) Calabria. "Ninafuraha kubwa kwa mashabiki wangu, najisikia fahari kwa timu hii ambayo kamwe haikukata tamaa.

"Tulifunga mabao ndani ya boxi, hivyo ni kweli kwamba kipindi cha kwanza hatukuwa kwenye wakati mzuri, lakini timu yote haikucheza vizuri na tulijua hilo.

"Tulionyesha morali kubwa sana baada ya mapumziko na sasa tumerudi rasmi kwenye kiwango chetu!

"Bado kuna safari ndefu mbele yetu. Bado tunaendelea kukimbia, lakini kuna mechi nyingi za kucheza na Inter bado wamebakia kuwa viongozi.

"Hivyo, tunatakiwa kushinda mechi zote na kuangalia nini kitakachofanywa na Inter."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
ATLETIC BILBAO
VERSUS
ESPANYOL
1 | 1.60
X | 3.90
2 | 5.60

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WILSHERE: ARTETA HANITAKI ARSENAL



**LONDON, England**

JACK Wilshere ameondoa uwezekano wa kurudi kwenye kikosi cha kwanza cha Arsenal, akisisitiza kwamba, kocha Mikel Arteta 'hamtaki' yeye.

Mchezaji huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya England, amekuwa mchezaji huru tangu alipoachwa na Bournemouth mwishoni mwa msimu wa 2020/21, lakini amekuwa akifanya mazoezi na 'Washikabunduki' hao hivi karibuni.

Mara ya kwanza alipoichezea klabu hiyo, kiungo huyo alicheza jumla ya mechi 200 na alishinda taji la FA mara mbili.

Akizungumza na Talksport, wakati alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kurudi kwenye kikosi cha Arsenal, Wilshere alijibu: "Kocha hanitaki mimi. Ndio, sidhani kama anataka hilo. Ningependa kurudi Arsenal. Lakini sina uwezo wa kuliwezesha hilo."

Arteta awali alisisitiza kwamba, kiungo huyo ataendelea kufanya mazoezi na klabu hiyo, lakini hakuna lolote litakalotokea.

"Nafikiri nilikuwa wazi kabisa kuhusu hali ya Jack na nafasi yake; ataendelea kufanya mazoezi tu."

Wilshere, ambaye hivi sasa ana umri wa miaka 30, amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa kubwa za Ulaya kwa kipindi cha mwezi uliopita, lakini hakuna dili lolote lililofanyika.

Lille walisemekana kuwa na mpango wa kumsajili Wilshere, lakini haraka uvumi huo ukafa wakati klabu hiyo ilipothibitisha ujio wa Hatem Ben Arfa.

# Lampard aanza kwa ushindi Everton

**LIVERPOOL, England**

FRANK Lampard alisherehekea siku "maalumu" kwake baada ya Everton kuifunga Brentford mabao 4-1 kwenye mchezo wake wa kwanza akiwa kocha wa kikosi hicho.

Lampard aliteuliwa kuchukua nafasi ya Rafael Benitez Jumatatu iliyopita, huku Dele Alli na Donny van de Beek pia wakiwasili hapo Goodison Park.

Na katika kuonekana ameanza kumaliza zama mbaya za Benitez, Lampard alianza kwa ushindi mtamu kwenye Kombe la FA Jumamosi na Everton imefuzu hatua ya tano ya mashindano hayo kwa mabao kutoka kwa Yerry Mina, Richarlison, Mason Holgate na Andros Townsend.

Albeit ambaye ni usajili mpya hakuwamo kwenye mchezo huo na Lampard alionekana kukunwa zaidi na matokeo hayo.

"Ilikuwa ni wiki ya aina yake, maalumu sana kwangu," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Ni siku ambayo kamwe sitaweza kuisahau. Ndio kwanza mwanzo wangu nikiwa hapa, lakini lazima nisema wazi kwamba, ulikuwa wakati wa aina yake kwa ushindi huu.

"Namna wachezaji walivyocheza kwenye mchezo huu na mashabiki walivyowapokea, inaonyesha kwamba, ni siku maalumu na ilikuwa maalumu zaidi kwangu."



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# RAGE ATAKA WENGINE KAMA MORRISON WAONDOLEWE SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Klabu ya Simba kumsimamisha winga wake, Bernard Morrison, kutokana na utovu wa nidhamu, kiongozi wa zamani wa klabu hiyo Ismail Aden Rage, ameunga mkono na kusema kama kuna wengine wapo kama mchezaji huyo waondolewe mara moja.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Rage alisema anawaunga mkono viongozi wa Simba kwa hatua waliochukua kwani klabu haiwezi kukaa na kumlipa mchezaji wa kigeni pesa za kigeni anayeshindwa kufuata masharti ya klabu.

"Naunga mkono kabisa, hatuwezi kukaa na wachezaji wa kigeni, tunamlipa pesa za kigeni, halafu hataki kufuata utaratibu wa klabu. Huo ni uamuzi sahihi na itakuwa ni fundisho kwa wengine," alisema Rage.

Kuhusu utovu wa nidhamu wa mchezaji huyo, Rage alisema hiyo ni hulka ya wachezaji wa Kiafrika anapoona yupo kwenye nchi ambayo ana soko na anapendwa na mashabiki wengi.

"Morrison ni mchezaji mzuri, ana uwezo, lakini isihalalishe kuwa ndiyo awe na nidhamu mbovu. Hii ni tabia ya wachezaji wengi wa Kiafrika hasa anapokuwa kwenye nchi ambayo ana soko na watu wanampenda, kwa Simba walichofanya ni sawa kwa sababu ikimwachia anaweza kuharibu tabia ya wachezaji wengine," alisema Rage.

Ijumaa jioni, klabu ya Simba ilitoa taarifa yake rasmi ya kumsimamisha mchezaji huyo kwa madai kuwa aliondoka kambini bila ruhusa ya uongozi na kwenda kusikojulikana.

Simba ilimsajili mchezaji huyo akitokea Yanga, na msimu huu anamalizia mkataba wake wa miaka miwili, huku taarifa za ndani zikidai kuwa klabu yake hiyo haitomwongeza mkataba, lakini tetesi zikidai huenda akarejea klabu yake ya zamani, Yanga.



Morrison

# Tenesi U-12 kupigwa Gymkhana Arusha

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya mchezo wa tenesi kwa vijana wenye umri chini ya miaka 12 (U-12), yanatarajiwa kufanyika Machi 12, mwaka huu, katika Klabu ya Gymkhana AICC jijini Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Olais Molel, alisema maandalizi yanaendelea vizuri.

"Maandalizi yanaendelea vizuri wachezaji wanaendelea na mazoezi kila siku kuelekea katika mashindano hayo," alisema Molel.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu zote za mchezo huo zilizoko Arusha pamoja na mikoa mingine.

Molel alisema anatarajia kuona mashindano hayo yatakiwa na ushindani mkubwa kwani kutokana na mikoa mbalimbali itakayotoa timu kushiriki kupania kufanya vizuri.

Aliitaja baadhi ya mikoa itakayoshiriki kuwa ni Dar es Salaam, Morogoro na Kilimanjaro.

Alisema kwa sasa mchezo huo umekuwa tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma kutokana na kila siku kuibuliwa vipaji vipya.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 07/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3363 | Sporting CP U23 vs CF Belenenses U23 | 1.92 | 3.62 | 3.29 |
| 15:00 | 4806 | Keshla FK vs Zira | 2.55 | 3.08 | 2.60 |
| 15:40 | 4556 | Alshoulla vs Najran SC | 1.77 | 3.18 | 4.53 |
| 16:00 | 2631 | Bright Stars vs Express FC | 3.66 | 3.13 | 1.97 |
| 16:00 | 2829 | Peterborough United Reserve vs Coventry U23 | 2.51 | 3.71 | 2.31 |
| 16:00 | 5410 | Charlton U23 vs Swansea U23 | 1.88 | 3.75 | 3.32 |
| 16:10 | 1919 | Bisha FC vs AL Nahdha | 2.45 | 2.84 | 2.94 |
| 16:30 | 5049 | Sassuolo Youth vs Atalanta Youth | 2.32 | 3.43 | 2.66 |
| 16:30 | 5296 | Bali Utd Pusam vs PSM Makassar | 1.55 | 3.61 | 5.59 |
| 17:00 | 1177 | East Bengal vs Delhi Dynamos FC | 3.28 | 3.66 | 1.92 |
| 18:00 | 1487 | Rio Ave U23 vs Leixoes SC U23 | 3.13 | 3.33 | 2.08 |
| 18:00 | 5558 | Neftchi Baku vs Karabakh | 3.77 | 3.38 | 1.86 |
| 18:05 | 2847 | AL Adalh vs Al Jabalain | 2.79 | 2.79 | 2.60 |
| 18:30 | 4621 | Porto B vs Covilha | 1.94 | 3.41 | 3.61 |
| 19:00 | 4583 | ASO Chlef vs CS Constantine | 3.12 | 2.79 | 2.37 |
| 19:00 | 4725 | Omonia Nicosia vs Ethnikos Achnas | 1.30 | 5.13 | 9.28 |
| 20:00 | 1237 | Hapoel Kfar Saba vs SC Kfar Qasem | 2.31 | 2.93 | 3.38 |
| 20:00 | 1250 | Penafiel vs CD Trofense | 2.08 | 3.27 | 3.36 |
| 20:00 | 3371 | Hapoel Petah Tikva vs Ahi Nazareth | 1.85 | 3.23 | 4.57 |
| 20:00 | 4184 | Doxa Katokopia vs Apollon Limassol | 8.92 | 4.76 | 1.34 |
| 20:00 | 4477 | Bnei Yehuda vs AS Ashdod | 1.99 | 3.36 | 3.71 |
| 20:00 | 4994 | USM Alger vs ES Setif | 1.75 | 3.45 | 5.00 |
| 20:00 | 5742 | Kocaelispor vs Boluspor | 3.84 | 3.46 | 1.82 |
| 20:30 | 4215 | Mamelodi Sundowns vs Chippa Utd | 1.36 | 4.21 | 9.21 |
| 20:55 | 1639 | Botosani vs Dinamo Bucuresti | 1.46 | 4.11 | 6.65 |
| 21:00 | 3913 | Saarbrucken vs Kickers Wurzburg | 1.59 | 3.92 | 5.10 |
| 21:00 | 5215 | Molynes vs Dunbeholden FC | 3.85 | 3.41 | 1.83 |
| 21:30 | 1403 | Oostende U21 vs Lommel U21 | 1.25 | 5.79 | 7.72 |
| 21:30 | 1554 | Charleroi U21 vs Anderlecht U21 | 5.18 | 4.61 | 1.45 |
| 21:30 | 2092 | St Truiden U21 vs Zulte Waregem U21 | 2.31 | 3.52 | 2.60 |
| 21:30 | 3232 | AS Eupen U21 vs Waasland Beveren U21 | 1.58 | 4.24 | 4.33 |
| 21:30 | 4332 | Maccabi Haifa vs FC Ashdod | 1.23 | 5.57 | 9.41 |
| 21:30 | 5738 | Resende RJ vs Audax Rio EC RJ | 2.27 | 3.09 | 2.99 |
| 22:00 | 1362 | Haladas vs Nyiregyhaza | 1.93 | 3.18 | 3.76 |
| 22:00 | 1697 | Jong Ajax vs Jong PSV | 1.70 | 3.80 | 4.29 |
| 22:00 | 2760 | Roda Kerkrade vs FC Volendam | 2.40 | 3.43 | 2.65 |
| 22:00 | 3626 | Tondela vs Benfica | 7.90 | 5.34 | 1.31 |
| 22:00 | 3935 | OH Leuven U21 vs Antwerp U21 | 1.57 | 4.60 | 4.90 |
| 22:00 | 4096 | FC Eindhoven vs SBV Excelsior | 2.51 | 3.39 | 2.56 |
| 22:00 | 4390 | Union Saint Gilloise U21 vs Beerschot Wilrijk U21 | 3.46 | 3.75 | 1.84 |
| 22:00 | 4392 | Kmsk Deinze U21 vs Lierse SK | 2.07 | 3.61 | 2.94 |
| 22:00 | 5728 | Jong Utrecht vs Helmond Sport | 2.24 | 3.42 | 2.89 |
| 22:30 | 2031 | RWD Molenbeek U21 vs Westerlo U21 | 2.23 | 3.72 | 2.61 |
| 22:45 | 2394 | Salernitana vs Spezia | 2.90 | 3.34 | 2.41 |
| 22:45 | 3713 | Paris FC vs AC Ajaccio | 2.37 | 2.94 | 3.14 |
| 22:45 | 5618 | Concarneau vs Villefranche Sur Saone | 2.01 | 3.17 | 3.66 |
| 23:00 | 2191 | Athletic Bilbao vs Espanyol | 1.60 | 3.90 | 5.60 |
| 23:00 | 2352 | Modena vs Cesena | 1.85 | 3.32 | 4.36 |
| 23:00 | 5006 | River Plate (URU) vs Mvo Wanderers | 2.27 | 3.19 | 2.90 |
| 23:15 | 5677 | Humble Lions FC vs Cavaliers FC | 5.59 | 3.85 | 1.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Februari 7, 2022
Nipashe



UKURASA 22

## Lampard aanza kwa ushindi Everton

NAKUJA...




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akiwa ameunasa mpira dhidi ya mabeki wa Mbeya City kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NABI ABEBA LAWAMA MECHI NA MBEYA CITY

●●●Aichambua huku akitoa sababu kuwashika, Lule afunguka mfumo na mbinu za kuishika...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikilazimishwa sare tasa nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anabeba lawama zote kutokana na matokeo waliyoyapata dhidi ya Mbeya City kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hiyo ni sare ya tatu Yanga inapata msimu huu huku ikiwa haijapoteza mechi hata moja kati ya michezo 14 iliyocheza hadi sasa wakati huu ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo juzi, Nabi kwanza aliwapongeza wachezaji wake kwa sababu walipambana kutafuta matokeo, lakini akiisifu Mbeya City kwa kufanikiwa kuzuia mipango yao na kuondoka na pointi moja.

"Katika mchezo huu siwezi kumtupia lawama mchezaji yeyote na lawaza zote nitabeba mimi za kutopata pointi tatu kwa sababu mchezo ulikuwa mgumu, wachezaji walipambana kutafuta matokeo, lakini wapinzani wetu walikuwa mahiri na kuharibu mipango," alisema Nabi.

Alisema timu zote hazikucheza vizuri kipindi cha kwanza na kipindi cha pili Yanga walicheza vizuri baada ya kubadilisha mfumo na kutengeneza nafasi nyingi lakini walishindwa kuzitumia.

"Tulitoa wachezaji ambao hawakucheza nafasi zao kama Dickson Job aliyecheza winga nafasi ambayo si yake, hii ni kutokana na Yassin Mustafa na wengine kuwa majeruhi.

"Kuhusu Feisal Salum kutoanza si sababu ya kutopata matokeo, Mbeya City walicheza kwa kufika miguuni mwa wachezaji na kuziba katika njia," alisema Nabi.

Alisema baada ya mchezo huo aliongea na wachezaji wake kwamba wasahau matokeo hayo na sasa wanaenda kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo huo kujiandaa na mechi ijayo.

Wakati Nabi akieleza hayo, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, naye pia anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kurejea nyumbani na pointi muhimu dhidi ya wenyeji wao, Yanga.

Lule alisema aliwasoma Yanga na kuona jinsi wanavyocheza, hivyo kuhakikisha wanaingia uwanjani kuharibu mipango ya wapinzani wao hao jambo ambalo walifanikiwa.

"Tuliwaheshimu na tulianza na mfumo wa 4-4-2, lakini kila muda unavyosonga tukabadilisha mfumo na kuingia na 4-3-3, kwa kuhakikishia tunawakaba Khalid Aucho na Zawadi Mauya ambao walikuwa kati," alisema Lule.

Alisema baada ya kufanikiwa kuwazuia nyota hao na kuifanya Yanga kutochocheza mpira wao na kuleta madhara langoni mwao, jambo ambalo walifanikiwa kuondoka na pointi muhimu licha ya kwamba mipango yao ilikuwa kubeba zote tatu.

"Niwapongeze wachezaji wangu kwa kufanya kile nilichowapa mazoezi na kukihamishia uwanjani, tuliwaheshimu Yanga kwa sababu wana wachezaji na benchi la ufundi zuri," alisema kocha huyo na kudai kwamba Ligi ya Tanzania hakuna timu kubwa bali Simba na Yanga ni sawa na timu zingine zinazoshiriki ligi hiyo.

## Waziri wa Fedha ataka VAR Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameahidi kumtafutia fedha Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengelwa kwenye bajeti ijayo ili kuweka Mashine za Msaada kwa Waamuzi (VAR) kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Waziri Mwigulu alitoa kauli hiyo jana kwa kuandika kupitia mtandao wake wa kijamii na Instagram, huku akiwa ameweka video ndogo ya mechi kati ya Yanga na Mbeya City iliyochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati timu hizo zikitoka suluhu.

Video hiyo fupi ilikuwa ikionyesha straika wa Yanga, Fiston Mayele akiwa anapokea pasi na mwamuzi msaidizi kuonyesha kuwa ameotea, wakati kupitia picha za marudio zikionyesha hakuwa ameotea.

"Nitaongea na waziri mwenzangu anayesimamia michezo bajeti ijayo tumtafutie fedha, tuweke VAR hata 10 viwanjani, tuweke nyasi bandia kuondoa utaratibu wa kucheza mpira shambani. Haya ndiyo maeneo yanayolalamikiwa, vinginevyo Yanga jana ilistahili kushinda."

Aliandika waziri huyo anayejulikana kuwa mpenzi wa timu ya Yanga.

Chapisho hilo lilipokelewa kwa hisia tofauti na mashabiki wa soka, wengine wakipongeza na baadhi wakipiga vijembe.

"Umesahau na ile penalti ya mchongo dhidi ya Namungo, VAR ingesaidia sana," aliandika mmoja wa mashabiki kwenye mtandao wake akisomeka kwa jina la Frank Donisio ambaye alijibiwa na Waziri Mwigulu.

"Zote sijasahau, nimegusa maeneo yanayolalamikiwa," Waziri alimjibu shabiki huyo wa soka.

Wengi walipongeza kuhusu wazo la kuwapo kwa VAR kwenye Ligi Kuu kwa sasa, lakini baadhi wakawa na mashaka kuwa limetoka wakati timu yake pendwa imenyimwa nafasi ya bao.

Wapo walienda mbali zaidi na kuandika kama VAR ikiletwa nchini, basi zitakazoathirika zaidi ni timu za Simba na Yanga kwa sasa kwani mara nyingi hunufaika zaidi na makosa ya kibinadamu ya waamuzi kuliko timu zote nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >